SUPA JACKPOT
TZS.1,139,859,317
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Jela** miaka 20 kwa kukutwa na meno ya tembo

UKURASA 2




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Agosti 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581393
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Mkandarasi mradi maji atozwa faini bil. 2.5/-

• **Kisa** ucheleweshaji mradi, kujiongezea mkataba kinyemela... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**WADAIWA SUGU KODI YA PANGO KUBANWA**
MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amezindua jengo la ghorofa 12 kwa ajili ya makazi...

UKURASA WA 4
**UWEKEZAJI KILIMO NA MIFUGO WAIPAISHA PSSSF NANENANE**
MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umesema maonyesho...

UKURASA WA 5
**WAZIRI: SOKO TANZANITE LITAITANGAZA TANZANIA KIMATAIFA**
WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula amesema...

## Miili ya ndugu waliofariki kwa ajali kuzikwa Dar, K'njaro

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Ujumbe Maalum wa Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, uliowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Wapigania Uhuru wa nchi hiyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ZANU-PF, Oppah Muchinguri Kashiri, Ikulu, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Uchakavu madarasa unavyoua ndoto za wanafunzi elimu bora

UKURASA 3



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda.

**MICHEZO** **YANGA:TUNAIFUATA NGAO YETU TANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akisikiliza kwa makini kuhusu elimu ya fidia kwa wafanyakazi iliyokuwa ikitolewa na Ofisa Mfawidhi Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Rose Satta alipotembelea maonyesho ya kimataifa ya wakulima Nanenane katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. Picha zaidi Uk. 8. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkandarasi maji aamuriwa kulipa bil. 2.5/- kwa ucheleweshaji mradi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAMPUNI ya Sogea Satom kutoka Ufaransa, inayotekeleza mradi wa maji wa Butimba, imetakiwa kulipa adhabu ya kisheria ya malipo ya Sh. bilioni 2.5 kutokana na kuzembea kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Licha ya kushindwa kukamilisha mradi huo kwa wakati, kampuni hiyo imedaiwa kuongeza kinyemela muda wa mkataba wa kufanya kazi hiyo bila uongozi wa mkoa kujulishwa.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa Mwanza, Amos Makalla, juzi alionyesha kukerwa na kitendo hicho licha ya kuahidiwa hivi karibuni kuwa mradi huo ungekamilika Julai 31, mwaka huu.

Makalla alisema kwa kushindwa kuheshimu mkataba na kuongeza muda kinyemela, aliagiza mkandarasi huyo kulipa fidia ya ongezeko la muda. Alisema mkandarasi huyo aliongezewa muda wa utekelezaji wa mradi huo kwa miezi mitatu mbele kinyemela ikiwa ni mara ya pili hali aliyosema haikubaliki na ni kinyume cha maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyetaka mradi huo kukamilika kwa wakati.

"Hiki kitendo narudia kusema hakikubaliki. Ni lazima mkandarasi huyu akatwe hiyo fidia ili fedha hizo zimuume kwani ni dhahiri hatambui wananchi wa Mwanza wanavyotaabika na kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu," alisema.

Makalla aliagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kukaa na Wizara ya Maji kuanza kutekeleza mara moja agizo la kumkata fedha hizo mkandarasi huyo kwa muda huo ili iwe fundisho kwa makandarasi wengine aliowaita wababaishaji.

"Hili jambo linashangaza sana. Mkandarasi amelipwa fedha kwa asilimia 100 na niliwaahidi wananchi kuanza kupata huduma ya maji ya uhakika kuanzia Julai 31 baada ya kuongezewa muda Februari, mwaka huu. Huyu Mkandarasi hana sababu yoyote ya kuongezewa muda lakini sasa ni lazima amalizie hiyo miezi 3 pamoja na adhabu hiyo malipo ya fedha. Kwa kweli sijaridhika kabisa," alisisitiza Makalla.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Robert Mhoja, aliahidi kutekeleza maagizo hayo na kueleza kuwa ifikapo Septemba 15, wananchi wa jiji la Mwanza wataanza kupata maji wakati mkandarasi atakapoanza majaribio. Alisema hatua hiyo itasaidia kutatua adha ya upatikanaji wa maji jijini Mwanza.

Sogea Satom ilianza kutekeleza mradi huo wa maji Butimba wenye gharama ya Sh. bilioni 70 mwaka 2021.

## Miili ndugu watatu waliofariki kwa ajali kuzikwa Dar, K'njaro

**Na Halfani Chusi**

NDUGU wanne wa familia moja waliofariki dunia juzi kwa ajali ya gari Chalinze mkoani Pwani, wanatarajiwa kuzikwa kesho na Jumanne.

Akizungumza kwa niaba ya kamati ya mazishi jana, Aminatha Juma alisema leo saa 6:00 mchana, watakutana Lugalo ilikohifadhiwa miili hiyo na kumuaga aliyekuwa dereva wa gari, Nechi Msuya, kaka wa wanafamilia na kisha kuanza safari ya kwenda Ugweno, Kilimanjaro keshokutwa.

Juma alisema baada ya maziko hayo, watakaokwenda Kilimanjaro, watarudi na wazazi Dar es Salam kwa ajili ya kuendelea na shughuli za maziko kwa wapendwa wengine, Sia, Nora, na Dayana.

"Baada ya hapo tutampeleka kwa pamoja, Dk Dayana Mageta nyumbani kwao Twangoma, Temeke na Agosti 8. Tutafanya ibada ya pamoja kwa kuwaaga wote watatu kwenye viwanja vya Gofu, Kawe kisha tutakwenda kuwazika katika makaburi ya Kondo Ununio.

Ndugu hao wanne walifariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso na Scania katika Kijiji cha Mapatano, Kata ya Mbwewe, Bagamoyo mkoani Pwani.

Ajali hiyo ilitokea saa 8:30 usiku kwa kuhusisha gari lenye namba za usajili T 104 CBU Toyota Prado lililokuwa likitokea Dar es Salaam kwenda Same, likiendeshwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Benki ya ABSA, Nechi Msuya.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi (ACP) Pius Lutumo, gari hilo liligongana na lori lenye namba za usajili T 881 DWU likiwa na tela lenye namba za usajili T888 DWU likiendeshwa na Philipo Mtisi (43) likitokea Arusha kwenda Dar es Salaam.

Lutumo alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa Toyota Prado kuhama kutoka upande wa kushoto kwenda kulia kisha kugongana uso kwa uso na lori hilo.

## Jela miaka 20 kukutwa na meno ya tembo

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKAZI wa kijiji cha Nalasi, Tunduru mkoani Ruvuma, Hemed Ally (35), amehukumiwa kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka 20 jela baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na nyara za serikali.

Ally alishtakiwa kwa madai ya kukutwa na meno ya tembo) bila kibali cha mkurugenzi wa Wanyamapori.

Wakati Ally akihukumiwa kutumikia kifungo hicho, mahakama hiyo pia imewaachia huru washtakiwa wawili waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka pamoja naye katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi baada ya kuwaona hawana hatia

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Tunduru, Honorius Kyando, baada ya upande wa Jamhuri ambao ulipeleka mashahidi watano, kuithibitishia mahakama bila kutia shaka.

Kyando alisema katika tukio hilo, mshtakiwa huyo alikutwa na vipande vinne vya meno ya tembo yenye uzito wa kilo 39.45 ambavyo thamani yake ni Sh. 34,700,440 200 mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema kitendo kilichofanywa na mshtakiwa huyo ni kinyume cha sheria za Tanzania, hivyo adhabu hiyo ni fundisho kwake na watu wengine ambao wamekuwa na tabia za kufanya vitendo vya ujangili dhidi ya wanyamapori na kutishia kutoweka kwa tembo.

Awali, akiwasomea shtaka katika kesi ya uhujumu uchumi namba 16/2022 mbele ya hakimu huyo, mwendesha mashtaka, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Thomas Zengo, alidai kuwa washtakiwa hao walikamatwa Agost 24, 2022 katika kijiji cha Wenje, Kata ya Mchoteka wilayani humo.

Alidai kuwa katika tukio hilo, Ally alinaswa na mtego huo baada ya maofisa Idara ya Wanyamapori kujifanya wanunuzi wa meno hayo.

Inspekta Zengo alidai kuwa kufanya hivyo, mshtakiwa alifanya kosa kinyume cha kifungu namba 86 (1) na (2)(b) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 Sura 283 ya mwaka 2009 ikisomwa pamoja na kifungu cha 14 cha jedwali la kwanza na kifungu namba 57 (1) na 60 (2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi na makosa yaliyopangiliwa sura ya 200.

Kabla ya kutiwa hatiani, mshtakiwa aliiomba mahakama impatie adhabu ndogo kwa vile ni kosa lake la kwanza na anategemewa na familia yake.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri uliiomba mahakama impatie adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine ambao wamekuwa wakifanya matukio hayo.

## HABARI KITAIFA

# Uchakavu madarasa unavyoua ndoto za wanafunzi elimu bora

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

NI giza katika ndoto za elimu bora. Ndivyo hali halisi ilivyo kutokana na uchakavu wa madarasa katika moja ya shule kongwe za msingi katika wilaya ya Kilolo mkoani Iringa.

Shule hiyo ya Kising'a iliyoko katika Kijiji cha Kising'a, tarafa ya Kilolo, ambayo inakabiliwa na uchakavu wa miundombinu ikiwamo baadhi ya madarasa kutokuwa na sakafu. Hali hiyo inawafanya wanafunzi kushindwa kuwa nadhifu.

Hivi karibuni Nipashe ilifika katika shule hiyo na kufanya mahojiano na baadhi ya walimu ambao hawakutaka majina yao kutajwa kwa vile si wasemaji.

Kwa mujibu wa walimu hao, licha ya shule kupata ufadhili wa ukarabati wa vyoo kutoka shirika la EPICO, madarasa mengi yamechoka na yanahitaji ukarabati wa sakafu huku wakiweka bayana kwamba kwa sasa uchakavu huo ni kikwazo katika ufundishaji na hata wanafunzi kuwa katika mazingira mazuri ya kujifunzia puia kuwa nadhifu.

Kutokana na hali hiyo, walimu hao waliomba wadau mbalimbali wa elimu kusaidia kuokoa jahazi ili kunusuru afya za wanafunzi hasa kutokana na mrundikano wa wanafunzi.

"Madarasa yakiwa na sakafu nzuri wanafunzi hawatachafuka na madawati yakiwa yanakaa vizuri hayatavunjika, lakini kwa hali ilivyo sasa, madarasa mengi hayana sakafu na wanafunzi wanachafuka," alisema mmoja wa walimu hao.

Mwalimu huyo alisema serikali iliwahi kutoa fedha za ajili ya ukarabati lakini ofisa elimu kata aliyokuwepo wakati huo, alibadilisha matumizi na kuelekeza katika ujenzi wa madarasa matatu.

"Kitendo cha kubadilisha matumizi ya fedha za ukarabati wa madarasa chakavu umepoteza malengo ambayo tulikuwa nayo kama shule," aliongeza mwalimu huyo.

Mwaka jana, shule hiyo yenye zaidi ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwake, ilikuwa na upungufu wa zaidi ya madawati 200 lakini kwa sasa umefikia madawati 160 baada ya kufanya harambee.

Kwa sasa shule hiyo ina wanafunzi 663 na walimu 13 na kwamba kutokana na sakafu kutokuwa nzuri, wanafunzi wanaugua kutokana na msongamano.

Afisa Elimu Kata (AEK) wa Kata ya Kising'a, Nasibu Chamwazi, alisema kutokana na uchakavu sakafu na madawati wanafunzi wanachafuka kwa sababu ya vumbi na kufanya wanafunzi kuwa wasafi siku moja kwa juma, hasa Jumatatu.

Chamwazi aliongeza kuwa wameshauriwa wazazi na walezi kununua sare zaidi ya mbili ili sare moja ikichafuka wavae nyingine, ikizingatia sehemu ya kata hiyo hali ni baridi.

"Tumependekeza ifikapo mwakani, wanafunzi wote wataanza kuvaa suruali ili kujikinga na baridi kali. Kama wanavyojua hali ya Kata ya Kising'a wilayani Kilolo ni baridi, hivyo wazazi wanatakiwa kununua sweta zaidi ya mbili," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Kilolo, Justin Nyamoga (kushoto), akichungulia katika moja ya madarasa yenye tatizo la miundombinu chakavu, alipotembelea shule ya msingi Kising'a hivi karibuni. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

Alisema mbali na uchakavu na uhaba wa madawati, changamoto nyingine ni uhaba wa walimu. Alisema Kising'a ina walimu 13 wakati mahitaji ni 17 na Shule ya Msingi Isele ina walimu tisa wakati mahitaji ni 11 ikiwa na wanafunzi 675.

### KAULI YA MBUNGE

Mbunge wa Kilolo, Justin Nyamoga, alitembelea shule hiyo na kujionea hali halisi na na kuahidi kulifikisha suala hilo kwa mamlaka husika.

Alisema lengo lake ni shule zote kongwe zikarabatiwe ili kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia na hatimaye kuongeza kiwango cha elimu wilayani hapa.

Shule hiyo ambayo ilianza mwaka 1972, ilifanyiwa ukarabati mara ya mwisho mwaka 1988, wakati shule ikiwa na mradi wa uvunaji miti.

Diwani wa Kising'a, Bora Kalinga, alisema Shule ya Msingi Kising'a, licha ya uchakavu wa madarasa, alikiri kwamba ina changamoto ya madawati. Alisema kata hiyo ina shule mbili ambazo ni Kising'a na Isele lakini kuna shule mbili shikizi zinaendelea kujengwa ambazo ni Kidumuka na Barabara Mbili.

Kalinga alisema kukamilika kwa shule hizo mbili (shikizi) zitapunguza mrundikano wa wanafunzi katika shule mama za Kising'a na Isele.

"Kwa mfano shule Mama ya Kising'a itakuwa na shule ya mkondo B ambayo iko katika Kijiji cha Kidumuka na Shule Mama Isele shule ya mkondo B ipo katika kijiji cha Barabara Mbili," alisema.

Shule shikizi hizo zitasaidia kupunguza idadi ya wanafunzi katika shule mama, zaidi ya wanafuzi 500 ambao kuanzia darasa la awali hadi darasa la tatu.

## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 67242 KIWANJA NA. '637', KITALU 'F' BUHONGWA MWANZA 3..NYUMBA YENYE HATI NA. 70437 KIWANJA NA. '213', KITALU '14' BUNJU KINONDONI , 4.NYUMBA YENYE HATI NA. 192019 KIWANJA NA. '130', KITALU 'N' PUGU MWAKANGA | 1. ZACHARIA ANTHONY KAPAMA 2. MARIANA ZACHARIAS BUKWIMBA 3.DAFROSA ATHONY KAPAMA 4. RASHIDI ALLY, | 1.KIFURU KINYEREZI-ILALA 2.BUHONGWA MWANZA 3.BUNJU KINONDONI 4.PUGU MWAKANGA | 22/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ITU COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 93457 KIWANJA NAMBA '1', KITALU 'G' MAPINGA ,KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 89175 KIWANJA NA. '1157', KITALU 'A' TEGETA KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA | ANDREW ANTHONY SINDABAHA | 1.MAPINGA BAGAMOYO 2.TEGETA | 11/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA | MPOKI BROWN MWAIPASI | KILUVYA | 17/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 23/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | DISMAS JEROME MALLYA | NYUMBA | EMMANUEL NAFTALI NGUVILA | SOKONI I -ARUSHA | 23/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EMMANUEL LEJASA KIMATH | NYUMBA | EMMANUEL LEJASA KIMATH | SINONI -ARUSHA | 23/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | IGNAS NDELILIO KAAYA | NYUMBA | IGNAS NDELILIO KAAYA | NKOANRUA -ARUSHA | 21/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | LABANI SAMSONI MAKALA | NYUMBA | LABANI SAMSONI MAKALA | SINONI- ARUSHA | 24/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EMANUEL DANIEL SORORWA | NYUMBA | FRANK THOMAS KIVUYO | OLTUMERET-ARUSHA | 28/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ALLEN MARTIN ISSANGYA | NYUMBA | ALLEN MARTIN ISSANGYA | AMBURENI-ARUSHA | 29/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | GODSON MELAYEKI MUNGURE | NYUMBA | GODSON MELAYEKI MUNGURE | AMBURENI - ARUSHA | 29/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | LESION JOSEPH MARTIN | NYUMBA | LESION JOSEPH MARTIN | SINONI- ARUSHA | 23/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | SIMON ANAEL SARAKIKYA | NYUMBA | SIMON ANAEL SARAKIKYA | NKOANRUA-ARUSHA | 21/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | JOSEPH LESSION LAIZER | NYUMBA | DICKSON EMMANUEL SOINE | SINONI- ARUSHA | 23/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | SIMON BOSCO KOISAN | NYUMBA | SIMON BOSCO KOISAN | SAMBASHA-ARUSHA | 21/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | PHILIPO ALOYCE ARISENI | NYUMBA | PHILIPO ALOYCE ARISENI | LEMARA -ARUSHA | 25/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | BEATRICE MOSES LEYARO | NYUMBA | BEATRICE MOSES LEYARO | BANGATA-ARUSHA | 21/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | NYUMBA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | MOSHONO -ARUSHA | 30/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | KADOGO LOMARATU | NYUMBA | KADOGO LOMARATU | KIMNYAKI-ARUSHA | 19/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MASANJA JAMES WANNA | KIWANJA | MASANJA JAMES WANNA | TERRAT - ARUSHA | 25/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | FELISTER JOHN KOSIANGA | NYUMBA | FELISTER JOHN KOSIANGA | OLTUROTO- ARUSHA | 25/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 11/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 17/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 25/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 22/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 22/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.NYUMBA (3) 2.KIWANJA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.IFWEKENYE -MBOZI 2.SONGWE | 21/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | JOSEPH RASHIDY MKONJA | NYUMBA (2) | 1.JOSEPH RASHIDY MKONJA 2.OLIVA YUSUPH MGENI | 1.SHEWA 2.MBALIZI | 23/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | NDIMBWELU BANDEKISYE KAFWENDA | NYUMBA | PAULO KALOTA NDAWILA | NZOVWE-MBEYA | 28/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI-MBEYA | 24/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BARAKA PAUL DABAVUNJE | NYUMBA | BARAKA PAUL DABAVUNJE | UYOLE | 29/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | NYUMBA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | IVUMWE | 30/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0745707008/0787129539/0759282344/0754376493/0759648448**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



Naibu Spika wa Bunge na Mbunge wa Jimbo la Ilala, Mussa Azzan 'Zungu', akizungumza katika mkutano wa hadhara wakazi wa Kariakoo, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo jimboni humo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Uwekezaji kilimo na mifugo waipaisha PSSSF Nanenane

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umesema maonyesho ya Nanenane yana maslahi kwa mfuko huo kutokana na uwekezaji ambao umefanywa kwenye maeneo ya kilimo na mifugo.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama, James Mlowe, alibainisha hayo jana 2023 kwenye banda la mfuko huo katika Maonyesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nanenane 2023) yanayofanyika kitaifa kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini hapa.

Alisema mfuko unayo majukumu manne ambayo ni kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza na kisha kulipa mafao.

"Katika eneo hili la Uwekezaji, Mfuko umewekeza kwenye maeneo mbalimbali mojawapo ni eneo la viwanda. Eneo hili tumewekeza kwenye kiwanda cha kuchakata Tangawizi, Mamba Miamba, Same mkoani Kilimanjaro na Kiwanda cha Chai Mponde, Lushoto mkoani Tanga," alisema.

Pia alisema PSSSF imewekeza kwenye machinjio ya kisasa ya Nguru, Mvomero mkoani Morogoro, kiwanda cha Kimataifa cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro (KLIC) na kwamba hiyo ni fursa kwa wafugaji.

Alisema kwa sababu hiyo, wakulima na wafugaji ni wadau muhimu wa PSSSF na kuwataka watumie maonyesho hayo kufika katika banda la PSSSF ili kujua fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mfuko katika maeneo hayo ya uwekezaji kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo.

"Hata kaulimbiu ya mwaka huu ya 'Vijana na Wanawake ni Msingi imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula' inatuunganisha. Tunapokuwa na chakula cha kutosha, tunajenga nguvu kazi imara ambayo ni vijana na hawa wanapoajiriwa serikalini wanakuja kuwa wanachama wetu.," alifafanua.

Akizungumzia ushiriki wa mfuko katika maonyesho hayo, alisema: "Hapa bandani ni ofisi kamili. Tunawahudumia wanachama wetu kama wanavyohudumiwa kwenye ofisi zetu zilizoenea nchi nzima Tanzania Bara na Zanzibar." Alisema wanachama wakiwemo wastaafu wakitembelea kwenye banda hilo, watakutana na watumishi na kuwahudumia na kupata taarifa kuhusu michango, mafao yatolewayo na mfuko, taarifa za uwekezaji na wastaafu kujihakiki kwa njia ya alama za vidole (biometric). Naye Mhasibu Mkuu wa PSSSF, Grace Kabyemela, aliwahakikishia wanachama, wakiwamo wastaafu kuwa mfuko uko katika hali nzuri ya kuhakikisha wanapata mafao yao kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

"Sheria inatutaka kuwa mwanachama anayestaafu anapowasilisha nyaraka zilizokamilika, anapaswa awe amelipwa mafao yake ya mkupuo ndani ya siku 60. Lakini sisi PSSSF tumejiwekea malengo ndani ya siku 30 tunafanya malipo," alibainisha.

Kuhusu malipo ya pensheni ya kila mwezi, Kabyemela alisema mfuko umejiwekea lengio kuwa ikifika tarehe 25 ya kila mwezi, wastaafu wanakuwa wamelipwa pensheni zao za mwezi.

Habiba Mhina, mwanachama wa PSSSF ambaye alitembelea banda la mfuko huo ili kupata taarifa za michango yake, baada ya kuhudumiwa alipongeza PSSSF kwa kumpatia taarifa zake kwa haraka

"Mimi ni mfanyakazi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma, nimefika banda la PSSSF kupata taarifa za michango na kwa kweli chini ya dakika teno nimepata huduma na kukabidhiwa taarifa ya michango yangu," alisema.

# Mhandisi halmashauri atumbuliwa kushindwa kusimamia miradi elimu

**Na James Mwanamyoto,** TAMISEMI

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Deogratius Ndejembi, amemwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Shadrack Mhagama kumchukulia hatua za kinidhamu Mhandisi Ujenzi wa Halmashauri hiyo, Daniel Kileo, kwa kushindwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya elimu.

Miongoni mwa miradi anayodaiwa kushindwa kuisimamia ni ujenzi wa madarasa ya mradi wa BOOST kinyume cha maelekezo ya serikali yaliyotolewa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Ndejembi alitoa maelekezo hayo juzi baada ya kutoridhishwa na ujenzi wa madarasa akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi inayojengwa na serikali kupitia miradi ya BOOST na SEQUIP.

Ndejembi alisema haiwezekani Rais Samia Suluhu Hassan atafute fedha za kujenga miundombinu ya elimu halafu zisitumike vizuri kwa sababu ya mhandisi wa wilaya kushindwa kutafsiri ramani wakati yeye ndiye mtaalam na mwenye jukumu hilo. "Mkurugenzi mchukulie hatua za kinidhamu mhandisi wa ujenzi na mkaimishe mwingine kwani huyu ameshindwa kusimamia ujenzi wa madarasa na Ofisi ya Rais TAMISEMI itakuletea mhandisi mwingine atakayesimamia miradi ya ujenzi ya miundombinu ya elimu," alisema.

Baada ya ukaguzi wa miradi ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Ndejembi amebaini kuwa miradi mingi katika Halmashauri hiyo haijakamilika wakati katika halmashauri zingine ikiwamo Manispaa ya Moshi imeshakamilika na changamoto kubwa kwa wilaya ya Moshi ikiwa ni kuwa na mhandisi ambaye ameonekana kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Aidha, Ndejembi alisema amepewa taarifa kuwa katika Shule ya Sekondari Ashira, bweni moja halijajengwa licha ya kuwa fedha zilitolewa na serikali na mhandishi huyo kushindwa kusimamia ujenzi huo.

# Wadaiwa sugu kodi ya pango kubanwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amezindua jengo la ghorofa 12 kwa ajili ya makazi na biashara lenye vitasa janja 'smart locks', vitakavyowabana wapangaji wasiolipa kodi kwa wakati kushindwa kufungua milango pale watakapodaiwa.

Akizungumza katika ufunguzi wa jengo la Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Dk.Mpango, alisema Tanzania ina upungufu wa zaidi ya nyumba milioni tatu, hivyo kukamilika kwa jengo hilo, kutapunguza tatizo hilo.

Dk. Mpango alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuweka mazingira wezeshi kwa TBA ili ijiendeshe na kupunguza utegemezi kwa serikali na kwa hatua hiyo ya ukamilishaji wa jengo hilo lenye uwezo wa kubeba familia 12, utasaidia kupunguza ruzuku kutoka serikalini na kujitegemea.

Aliagiza sekta binafsi kushirikiana na TBA katika ujenzi wa nyumba ikiwamo wakala kujenga ghorofa maeneo yaliyorejeshwa serikalini ili kuondokana na changamoto ya makazi nchini.

Mradi huo, alisema umezingatia ubunifu ikiwamo wataalamu waliohitimu vyuo vya ndani kwa ajili ya kuwapatia uzoefu na ujuzi kwa vitendo na kupongeza uwekaji wa mfumo wa vitasa janja ambao utakuwa ni suluhisho la ulipaji wa kodi za pango kwa wale wasumbufu

"Mradi huu umechochea uzalishaji katika viwanda vya vifaa mbalimbali vikiwemo vifaa vya saruji, bati na kuongeza mapato kwa wazawa watakaozalisha vifaa hivi,"alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, hivi sasa serikali inafanya tathimini kwa mashirika na taasisi za umma zisizozalisha ili kuyafuta.

"Nawapongeza TBA mpo kwenye njia sahihi ya kuondoka kwenye utegemezi wa ruzuku ya serikali kwani sasa mtaingiza mapato kupitia majengo haya ya biashara mnayojenga na wengine waige mfano huu ili waondokane na mkono wa chuma wa kuja kuyafuta," alisema.

Makamu wa Rais aliwaagiza wapangaji wa nyumba hizo kutunza mazingira na kuzingatia masharti ya mikataba ikiwamo ulipaji wa kodi kwa wakati ili kuondokana na adha ya kufungiwa milango hiyo ya vitasa janja.

Kadhalika, aliagiza TBA itunze mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yote inayojenga nyumba ikiwamo kukidhi mahitaji ya soko na kuvuna maji ya mvua ili kumwagilia miti na maua yaliyopo kwenye majengo yao.

Akitoa taarifa ya mradi wa jengo la makazi la kibiashara lililopo katikati ya barabara ya Kinana na Afrika Mashariki eneo la Sekei, Msanifu wa jengo hilo, Daud Kondoro, ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa TBA, alisema lengo la mradi huo ni kuwezesha wakala kujikwamua kiuchumi na mapato hayo yatasaidia kuondokana na utegemezi wa serikali kuu.

Alisema mradi umetekelezwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 6.665 na umetekelezwa kwa awamu nne hadi kukamilika kwake kutoka mwaka 2007 hadi 2023. Aisha alisema wanatarajia kukusaya Sh.milioni 210 kila mwaka na mapato hayo yatawawezesha kujikwamua kiuchumi. Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makamo Mbarawa, alisema ujenzi huo umezingatia ubunifu ikiwamo uendelezaji wa ujenzi wa nyumba katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wameweka mfumo huo wa vitasa janja kwaajili ya kudhibiti kodi ya pango na kuhimiza watu kulipa kwa wakati ili kuondokana na kufungiwa milango.

HABARI KITAIFA

# Waziri asema soko la tanzanite litaitangaza Tanzania kimataifa

**Na Munir Shemweta,** MIRERANI



WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (pichani) amesema kuwapo kwa soko la madini nchini kutaifanya Tanzania kujulikana zaidi na kukaribisha watu kutoka nje ya nchi.

Dk. Mabula aliyasema hayo juzi alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa soko la madini ya Tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara.

Ujenzi wa mradi wa soko hilo unatekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) chini ya mshauri Chuo cha Ufundi Arusha kwa gharama ya Sh. bilioni 5.49.

"Tuna imani hata wafanyabiashara wa madini kutoka Tanzania sasa watalinda rasilimali za nchi na kuhakikisha muuzaji mkubwa wa madini ya tanzanite ni yule anayetoka kwenye nchi yake pamoja na kuwa na soko," alisema Dk. Mabula.

Aliwataka wamiliki wa soko hilo la madini ya Tanzanite kuona namna bora ya kujitangaza zaidi ikiwamo kutumia tovuti huku wakionyesha kuwa soko hilo liko Tanzania na Mererani ambako ndiko madini yanakochimbwa.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, matangazo ya soko hilo yanaweza kuanza mapema wakati ujenzi ukiendelea ili ifahamike kuwa madini hayo yanapatiakana nchini na soko lake liko Mererani jambo alilolieleza litaongeza juhudi za kulinda rasilimali za nchi.

Alimpongeza mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro na timu yake kwa kuwa na wazo la kuwa na soko la madini ya Tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani.

Alisema uamuzi huo utafungua fursa kwa Watanzania lakini pia kwa nchi.

Awali, Meneja wa NHC Mkoa wa Kilimanjaro, Juma Kiaramba, alimweleza Waziri Mabula kuwa ujenzi wa soko hilo ulianza rasmi Mei 22, 2022 na unatarajia kukamilika mwezi Oktoba, mwaka huu.

Kiaramba alisema ujenzi wa mradi huo unaendelea vizuri ingawa shirika linakabiliwa na changamoto kubwa ya kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

Hata hivyo, alisema katika kukabiliana na hali hiyo, shirika limekuwa likinunua vifaa vikubwa kutoka vyanzo vya uzalishaji na kutolea mfano wa nondo na saruji ili kuhakikisha gharama za ujenzi zinabakia kama zilivyo.

# Mashirika yaungana kupiga vita rushwa

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI Mtendaji wa HakiRasilimali, Adam Anthony, amesema mpango mkakati wa mashirika binafsi kuungana pamoja kuisaidia serikali kupiga vita rushwa umeiva na kwamba muda wowote utaanza kazi.

Anthony aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, katika hafla iliyowakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa ajili ya kuandaa mkakati wa kukabiliana na vitendo hivyo.

Alisema wameamua kuandaa mkakati wa pamoja, ili kuisaida serikali kupambana na rushwa jambo alilodai serikali pekee haiwezi kumaliza tatizo hilo.

Pia alitahadharisha kuwa rushwa ni adui wa haki na kama isipokemewa inaweza kulirudisha nyuma taifa na kuangukia katika dimbwi la umaskini na kuwaacha wachache wakinufaika.

"Hatuwezi kukata tamaa. Dira yetu ni kuongeza zaidi uwazi na uwajibikaji bila kusahau kupambana na vitendo vya rushwa ndani ya mashirika yasiyo ya kiserikali, tunaamini kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeisaidia serikali kwa kiasi kikubwa sana kwa kuwa rushwa sio jambo la kuiachia serikali pekee.

"Kipindi cha nyuma kila asasi ilikuwa inafanya hayo peke yake, lakini kwa sasa tumeona tuungane pamoja kupaza sauti tunaamini hii inaweza kuwa tiba katika maeneo ambayo tunayasimamia," alisema.

Awali, Msimamizi wa Mtandao unaotoa Elimu ya Uraia Tanzania, Mobelo Kaiza, alisema mkakati huo utaleta tija kwa kuwa umesheheni mambo mengi ambayo yanaweza kuwa suluhu ya tatizo hilo pamoja na kuchochea uwazi na uwajibikaji nchini.


RAFIKI - SDO

**Tender No: RAFIKI-SDO/KAGIS/FY23/TND/01.**
**Supply of Reusable Sanitary Pad.**

**Issue date: 31st July 2023**
**Questions and clarification: Due by 7th August 2023;**
**Closing date and time: 13th August 2023; 17:00 PM**
**Date of solicitation: 14th August 2023**

**Introduction**
Rafiki Social Development Organisation (RAFIKI-SDO) is a Non- governmental and Nonprofit making organization working with children, youth, marginalized and vulnerable groups, families and their communities to reach their full potential by advocating their rights and tackling the causes of poverty and injustice. The organization was established in 2005 and registered under NGO Act of 2002, issued with registration number No.00NGO/R1/00903 to operate in Tanzania Mainland. Visit us at**www.rafikisdo.or.tz**

Rafiki-SDO is implementing the Keeping Adolescent Girls in School Project in Geita region which is funded by Global Affairs Canada (GAC) through Plan International Tanzania with the aim to address key barriers inhibiting adolescent girls from realizing their right to safe, quality and gender-responsive education, with a particular focus on their unique needs and barriers associated with participation in primary and lower-secondary school. The project's Ultimate Outcome is whereby 'Adolescent girls realize their rights to safe, quality, gender-responsive education' will be achieved by employing a three-pronged, rights-based, gender-transformative approach to tackle demand- and supply-side barriers, while strengthening local level governance and building improved linkages between education, health and child protection systems.

**Objective of the Assignment**
The overall objective of this assignment is to procure and distribute reusable sanitary pad 10,250 packets to Rafiki-SDO for adolescent girls.

**Delivery will be at our offices Geita region.**

| Item | Description of the item | Number of items per packet |
|---|---|---|
| Pad | **Reusable Sanitary pad**, (Relief pad,enriching the lives of women around the world) | **4 pieces** |

Interested vendors should download the full terms of reference through **www.rafikisdo.or.tz**

All questions and request for clarification should be directed to: **procurement@rafikisdo.or.tz** with the subject line **"Request for Clarification Supply of Reusable pad.**

**Eligibility**
To be considered for the award, Vendor must be currently legally operating in Tanzania and the quotation must include all the following information:
- Ability to meet specifications outlined above.
- Ability to deliver the items no later than the date(s) required.
- Legally registered in Tanzania.

**Evaluation Criteria:**
- Legal eligibility
- Technical capacity/ experience.
- Price.
- Quality of items to be supplied (Shortlisted applicants will be required to submit samples).

**Submission Instructions**
Interested dealers must submit the following information to RAFIKI-SDO:
1. Current company profile.
2. Copies of registration certificate and address of their registered office, valid business license, VAT(if applicable), TIN certificates, and valid Tax clearance certificate
3. Items specifications are fully addressed in the quotation.
4. Payment terms 100% after delivery.
5. Evidence of similar assignments, and at least two (2) names and addresses of client served.
6. Deliver time must be specified.
7. Quote valid for atleast 90 days.
8. Interested vendors should visit RAFIKI-SDO office to see a Reusable pad sample before submitting a quote (shortlisted vendors will be required to submit samples similar to or close to the sample provided by RAFIKI-SDO).

Vendors who wish to apply for this tender should send their proposal in sealed envelopes to Rafiki-SDO Geita Office not later than **13th August 2023, 17:00 PM.**

All sealed envelope need to be marked as **"Tender for Reusable sanitary pads"**

**Office address:**
The tender committee Rafiki-SDO
Katoma street,Kalangalala ward.
P.O Box 194, Geita.
Rafiki-SDO will open all bids on **14th August 2023 at 14:00 PM** in presence of bidder's representative who choose to attend.

Quotes must be in Tanzanian shillings and include VAT separately if applicable:

Proposal submitted through email will not be considered.

Quotation received after the time or at different address may not be accepted

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi Simba wawaweke wazi mashabiki

**KESHO** ndio kilele cha tamasha la klabu ya Simba maarufu kama 'Simba Day' ambapo mashabiki watapata fursa ya kuangalia wachezaji wao wapya waliosajiliwa kwa ajili ya msimu ujao wa ligi na mashindano ya kimataifa.

Ni siku ya furaha kwa kila mwana Simba, ni siku ambayo wanapata picha ya timu yao kuelekea kwenye mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Pamoja na kuwa ni wiki ya shamrashamra kwa Simba, lakini si vibaya kuwakumbusha viongozi wa klabu hiyo kuhusu mambo mengine ya maendeleo ya timu hiyo.

Tunafahamu kwa muda mrefu kulikuwa na mchakato uliokuwa unaendelea wa uwekezaji wa timu hiyo, jambo ambalo kwa muda mrefu lilionekana kusimama huku mashabiki, wanachama na wadau wa soka hapa nchini wakiwa hawafahamu nini kinaendelea.

Juzi tume ya ushindani wa kibiashara hapa nchini (FCC) kupitia kwa Mkuregenzi Mtendaji wake Williams Erio ilitoa maelezo juu ya suala hilo la uwekezaji wa klabu ya Simba.

Taarifa hiyo ya FCC imeibua maswali mengi kwa wadau wa soka hapa nchini.

FCC imeeleza kuwa katika mchakato huo wa uwekezaji, upande ambao umeonekana kuwa na shida ni upande wa wanachama wa klabu hiyo.

Inafahamika uwekezaji katika klabu ya Simba ni wa pande mbili, kwa maana ya muwekezaji ambaye ni Mohamed Dewji 'Mo' na upande wa mashabiki wa klabu hiyo.

Siku za nyuma ilionekana kama mchakato huo unakwamishwa na mwekezaji, Mo, lakini kwa kauli ya FCC ni wazi upande wa Mo hauna shida kwenye uwekezaji huo na tatizo lipo upande wa klabu kwa maana ya mashabiki.

FCC imeweka wazi kuwa Mo alikamilisha taratibu zote alizotakiwa kuzifuata, lakini kikwazo kipo upande wa mashabiki ambao taarifa inasema walipaswa kuwasilisha hati za mali.

Katika hili uongozi wa klabu unapaswa kuweka wazi kwa mashabiki nini kimepelekea suala hili kukwama, nini kimefanya hati hizo kutowasilishwa kwa wakati na matakwa ya kisheria katika uwekezaji waliolenga kuufikia.

Katika bodi ya klabu hiyo, upande wa mashabiki unawakilishwa na Mwenyekiti Murtaza Mangungu na wajumbe na upande wa mwekezaji pia kuna wajumbe wake.

Mangungu kama Mwenyekiti wa klabu hiyo anapaswa kuwaambia ukweli wanachama wa klabu hiyo wapi hasa mchakato umekwamia, nini kimepelekea kushindwa kutimiza masharti waliyopaswa kutimiza.

Ni zaidi ya miaka sita sasa tangu mchakato huu uanze, lawama nyingi zimekuwa zikienda kwa mwekezaji kwa madai ya kukwamisha kwa makusudi mchakato huu,lakini hata hivyo FCC imekuja kuibua jambo lingine.

Wanachama wa Simba wanataka kujua wapi mchakato umefikia, Mangungu na viongozi wenzake wanapaswa kuwageukia wanachama na kuwaambia wapi wamekwama ili waweze kujikwamua na kusonga mbele.

Kukaa kimya bila kutoa taarifa yoyote ni kuwakosea wanachama wao ambao wana haki ya kujua kila jambo linalotokea katika klabu yao hiyo.

Hata kama suala hilo litakuwa mbele ya wadhamini wa klabu hiyo, basi Mangungu anapaswa kuwaambia wanachama ili kwa pamoja wapate ufumbuzi wa mkwamo uliopo sasa wa kukamilisha mchakato huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Bodi ya Ligi itoe hata ratiba ya ufunguzi tu

Na Adam Fungamwango

**LIGI** Kuu Tanzania Bara inatakiwa ianze Agosti 15 kama ilivyotangwaza awali na Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Hata hivyo, ikiwa imebaki takriban siku 10, ratiba haijatoka na kuwashangaza wadau wa soka na mashabiki wake.

Hiyo ilimfanya Afisa Mtendaji Mkuu Almasi Kasongo kuja kwenye vyombo vya habari na kutaja kile kilichosababisha mpaka leo ratiba ichelewe.

Kasongo alidai kuwa bado Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) halijatoa kalenda yake rasmi ya mashindano ya mwaka mzima.

Akasema walikuwa wanasubiri ratiba hiyo ya CAf ili kupanga ratiba yao kutokana na uwakilishi wa klabu nne kwenye mashindano hayo ya CAF hivyo walikuwa wanaogopa kuchanganya ratiba za timu hizo.

Akasema iwapo watapanga ratiba wanavyotaka wao bila kwanza kuiangalia ya CAF, zinaweza zikasababisha tarehe za mechi za michuano ya CAF na za ligi kuingiliana.

Kuna maswala ya usafiri kwani ratiba inaweza kuonyesha timu inacheza mechi ya ligi, lakini inatakiwa isafiri siku hiyo kwenda kucheza nje ya nchi.

Timu za Tanzania zinazoshiriki michuano ya kimataifa ni Simba, Yanga, Azam FC na Singida Fountaine Gate.

Kasongo alisema timu hizo ambazo pia zitacheza Ligi Kuu Tanzania Bara zinahitaji ratiba rafiki ili ziiwakilishe vyema nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Mbali na michuano ya klabu za Tanzania, kuna michuano ambayo Simba inashiriki peke yake ya Super League, pia kukiwa na mashindano ya timu za taifa kama kusaka tiketi ya kufuzu Kombe la Dunia, AFCON na mingine mingi.

Kwanza kabisa nakubaliana na Bodi ya Ligi kuwa haiwezi kupanga ratiba vizuri kabla ya kuangalia ratiba nzima ya CAF, ndiyo nao wafanye hivyo.

Huko nyuma tuliona malalamiko kwa baadhi ya klabu zikidai kuna timu zinabebwa kwa sababu tu mechi zao zimeahirishwa ili zisafiri kwenda nje ya nchi kuwahi pambano la kimataifa.

Licha ya malalamiko, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa ligi inakuwa na viporo vingi na timu inayozidi kusonga mbele zaidi kwenye mashindano ya CAF ndiyo mechi zao nyingi zinaahirishwa.

Naipongeza Bodi ya Ligi kwa kutoingia kwenye mtego huo ambao baadaye unazaa lawama kwa sababu timu zinazotoka mapema zinaanza kuzilalamikia zinazosonga mbele.

Pamoja na hayo, Bodi ya Ligi angalau ingetoa ratiba ya timu zitakazocheza mechi ya ufunguzi ili kila mmoja ajue anacheza na nani.

Vinginevyo basi inabidi itangaze kuahirishwa kwa tarehe ya kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kutotangaza ratiba kunawanyima hata makocha kupanga mipango mikakati ya kucheza mechi zao.

Isidhaniwe kuwa makocha wanafundisha tu stamina, pumzi na mifumo peke yake. Hufundisha pia kumkabili mpinzani wanayekwenda kucheza naye.

Mfano kocha wa Prisons akijua ataanza na Yanga, basi anawatengeneza wachezaji wake kupambana na jinsi wapinzani wanavyocheza.

Mashujaa FC watapewa mfumo wa kuikabili Simba, kocha akiwaelekeza jinsi ya kucheza kama ukitaka kuwadhibiti wachezaji wake.

Hilo ndilo Bodi ya Ligi walipaswa walijue, lakini hadi leo hakuna timu yoyote inayojua itacheza na nani, kiufundi wala siyo sawa.

Kwa hiyo wakati wawasubiri CAF, Bodi ya Ligi nawashauri wafanye mambo mawili tu, watoe angalau ratiba ya ufunguzi ili kila mmoja ajue atacheza na timu gani makocha wajue jinsi ya kukabiliana, au waahirishe hadi hapo mambo yatakapokaa sawa.

# Majaliwa ataka mapato ya kilimo, mifugo kuendeleza sekta husika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa ameitaka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuhakikisha mapato yanayotokanao na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yanatengwa na kutumika katika kuboresha sekta hizo.

Majaliwa alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na wadau na washiriki baada ya kukagua mabanda ya Maonyesho ya Nane Nane Kitaifa yanayoendelea kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya.

"Ofisi ya Rais (TAMISEMI) hakikisheni mnasimamia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 unaozitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga mapato ya ndani yatokanayo na tozo mbalimbali kwenye mazao ya kilimo (asilimia 20), mifugo (asilimia 15) na uvuvi (asilimia 5) zinarudi na kutumika kuboresha sekta hizo ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa mazao ya kimkakati," alisema.

Ili kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo, uvuvi na mifugo, Waziri Mkuu aliwataka wadau wa sekta hizo wazitumie taasisi za fedha nchini kupata mikopo itakayowasaidia kuongeza tija na kuendeleza biashara zao.

"Taasisi za fedha zimefungua dirisha kwa ajili yenu, wanataka wawasikie. Hakuna maendeleo bila kukopa, lakini ni lazima vigezo na masharti vizingatiwe. Unapotaka kufanya maendeleo ukakosa mtaji, nenda kakope lakini ukikopa mwisho wake lazima urejeshe ili na wengine waweze kukopa," alisisitiza.

Aidha, Majaliwa alisema kuwa serikali imeendelea kufanya mazungumzo na taasisi mbalimbali za fedha ili kushusha riba kwenye mikopo zinazotoa na kuongeza fursa kwa wajasiriamali nchini ili wapate mikopo na kuendeleza shughuli zao na kuwa na tija.

"Nimefurahi sana kukuta baadhi yao wameshusha riba mpaka asilimia tisa.

Ni matumaini yangu watashuka zaidi," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliwaagiza wakuu wa mikoa na viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kushirikiana na wizara husika kuhakikisha vijana wanapatiwa maeneo ya mashamba, mafunzo na kuwatafutia wadau watakaowasaidia kupata mitaji ya kuendesha shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi na masoko ya uhakika.

"Ninawaagiza wakuu wa mikoa mshirikiane na mamlaka za serikali za mitaa katika maeneo yenu kuhakikisha wanatenga maeneo ili vijana wanaopata mafunzo ya BBT (mpango wa kuwawezesha vijana kulima, kufuga na kuvua samaki kibiashara) wakute yako tayari.

Tunataka hawa vijana wakitoka kwenye mafunzo, wakute maeneo yako tayari na waanze kazi mara moja," alisisitiza.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke Dar es Salaam, Mobhare Matinyi (wa pili kulia) na timu yake wakitembelea bandari kavu (ICD) ya kampuni ya HESU iliopo wilayani humo, kujionea jinsi inavyofanya shughuli zake na kuangalia changamoto zake. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Walia upatikanaji pembejeo kwa wakati

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKULIMA wameiomba serikali kuangalia namna ya kuwasaidia kupata pembejeo za kilimo kwa wakati ili kupata mazao mengi, bora na kuendana na wakati uliopo.

Rai hiyo ilitolewa jana na mmoja wa wakulima, Nipa Msangi, alipotembelea maonyesho ya 30 ya Wakulima Kanda ya Mashariki yanayofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, mjini hapa.

Msangi alisema serikali inajitahidi katika upatikanaji wa pembejeo za kilimo lakini bado changamoto hiyo haijaisha ikiwamo ukosefu wa mbolea kupitia kwa mawakala wanaotegemewa. Pia alisema kuna mazao kama mahindi lishe ambayo yanaonekana yanaweza kuwainua kiuchumi baada ya kulima tofauti na mahindi ya kawaida lakini wanashindwa kulima kutokana na ukosefu wa zana bora za kilimo.

Ofisa Masoko wa Kampuni ya Africasia Seeds ya Arusha, Godfrido Urassa, alisema watu wengi kwa sasa wanakimbilia katika kilimo cha mahindi lishe yajulikanayo kama 'dhahabu tamu' kutokana na kuwa na baadhi ya madini.

Urassa aliiomba serikali kuangalia changamoto ya mbolea iliyoko licha ya kuwapo kwa ruzuku sambamba na kuogeza mawakala wa kusambaza mbolea hizo kwa sababu waliopo ni wachache na kufanya wakulima wengi kukosa mbolea.

Alisema mbolea ndicho chakula cha mmea na ili mmea ukue, unahitaji mbolea ya kutosha na ndipo utatoa mazao mazuri na mengi kulingana na maelekezo ya mmea husika.

Ofisa huyo aliwashauri wakulima wanapokosa mbolea za madukani kuona umuhimu wa kutumia mbolea za kienyeji kama vile samadi na mboji ili kustawisha mimea na kupata mazao.

Aliwataka wakulima kujikita kwenye kilimo cha mahindi lishe ambacho kinatumia mbegu kilo moja pekee yenye thamani ya Sh. 200,000 ambayo hutosha kwenye eka moja na kupata magunia 20 tofauti na mahindi ya kawaida ambayo hupandwa kilo nne kwa eka moja mavuno huwa kidogo.

## TARI yawaita wananchi kujifunza kilimo

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANANCHI wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma wameombwa kutembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Naliendele kwenye Maonyesho ya Nanenane 2023 yanayoendelea viwanja vya Ngongo, mjini hapa kupata teknolojia za kilimo bora cha kisasa.

Ombi hilo lilitolewa na Mratibu wa Uhawilishaji Teknolojia na Uhusiano, Bakari Kidunda, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari katika maonyesho hayo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa TARI Naliendele, Dk. Fortunus Kapinga, Kidunda alisema taasisi hiyo imejipanga vizuri kwa wakulima wategemee kupata ujuzi mkubwa kwenye masuala ya kilimo katika maonyesho hayo.

Kidunda alisema kituo kinatarajia kuonyesha teknolojia za kilimo za kuvutia wakulima kutoka mikoa hiyo ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambao wanaombwa kujitokeza kwa wingi kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo za kisasa na bora.

Alisema TARI Naliendele ni moja ya vituo 17 vilivyo chini ya TARI na kwamba wanavyo vingine kama hivyo katika kanda zingine nchini ambazo jukumu kubwa ni kuhakikisha teknolojia zinawafikia wakulima bila ya matatizo.

Pia alisema TARI Naliendele imepewa jukumu la kitaifa kutafiti mazao ya korosho, ufuta na karanga kutokana na changamoto zinazojitokeza kwenye mazao hayo, hivyo inawajibika na majukumu ya kutoa majibu.

Kidunda alisema wamekuwa wakifanya utafiti wa mazao mengine kwa kushirikiana na vituo vingine vilivyopewa mamlaka kitaifa na kwamba katika maonyesho hayo, wana program ya utafiti wa nafaka za mikunde, jamii ya mizizi, mboga na matunda.

Kwa mwaka huu, alisema wamejipanga vilivyo kuonyesha teknolojia zote za kilimo na litakuwa tukio la aina yake kwa kuwa wale waliozoea kufika kwenye Nanenane Ngongo, wataona shughuli endelevu za kituo hicho kwa kuwa wanafanya maboresho mbalimbali ya ya kisasa kila idara.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza katika viwanja hivyo, wamepongeza kazi inayofanywa na taasisi hiyo na kuishauri mafunzo ya aina hiyo yasisubiri hadi ufike msimu wa Nanenane ndipo yafanyike bali yawe endelevu.

HABARI PICHANI

# MAONYESHO YA WAKULIMA NANENANE KATIKA PICHA



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa tatu kushoto), akifurahia muziki alipotembelea mabanda ya maonesho ya kimataifa ya wakulima Nane Nane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkuu wa wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (kulia), akiangalia mafuta yatokanayo na mbegu za zao la tango, alipotembelea banda la halmashauri ya wilaya hiyo katika maonyesho ya wakulima Nanenane jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka akipata maelezo na historia ya John Mwakangale kutoka kwa Mratibu wa Kumbukumbu za John Mwakangale, Christina Mwakangale (kulia), baada ya kutembelea katika maonyesho ya kimataifa ya wakulima Nanenane jijini Mbeya, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wilaya ya Bahi, Siwajibu Selemani (kulia), akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea shamba darasa kwa ajili ya kujifunza kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane Kanda ya Kati, katika Uwanja wa Nzuguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkuu kutoka Idara ya Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais, Zanipha Msangi (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari JM Kikwete ya Tunduma mkoani Songwe, walipotembelea maonyesho ya kimataifa ya wakulima Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya jana. **PICHA: OMR**



## HABARI DODOMA

# Bahi yapigia debe uwekezaji viwanda

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bahi imetoa wito kwa wawekezaji wa sekta za kilimo,mifugo, uvuvi na bidhaa mbalimbali kujenga viwanda wilayani humo kutokana na kuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji huo.

Ofisa Kilimo, Uvuvi na Mifugo Wilaya ya Bahi, Siwajibu Seleman, alitoa rai hiyo jana kwenye Maonyesho ya Kilimo, maarufu kama Nanenane Kanda ya Kati yanayoendelea jijini hapa.

Alisema sekta hizo bado zinahitaji wawekezaji hao watakaosaidia kuwainua wakulima, wafugaji na wavuvi wa wilaya hiyo kiuchumi.

Uwapo wa viwanda wilayani humo, alisema utaongeza uhakika wa wakulima kulima mazao mengi yenye tija na kwa upande wa uvuvi na ufugaji utawaongezea soko la uhakika na kuondokana na hofu ya kuharibika kwa bidhaa zao.

Alisema kuna wakati wavuvi ,wafungaji na wakulima wanatamani kuongeza bidii kwenye sekta hizo lakini wana hofu kupoteza nguvu zao, njia pekee ya kuwaokoa ni kuwepo viwanda vya usindikaji hali itakayowainua kiuchumi na kuwa na maisha bora.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii na Vijana wa Wilaya hiyo, Dennis Komba, alisema ili kufanikiwa kwenye masuala ya uwekezaji na masoko, wamejipanga kuwanufaisha vijana, wanawake na wenye ulemavu kulima kilimo biashara na kuongeza thamani ya mazao.

# Uvuvi haramu watishia samaki kutoweka

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Paskasi Mulagiri, amebaini hatari ya kuua kizazi cha samaki kwenye maziwa ya Kindai na Singidani kutokana na uvuvi haramu.

Kutokana na hali hiyo, amepiga marufuku wavuvi kutumia nyavu ambazo haziruhusiwi na watakaobainika watafikishwa mahakamani.

Mulagiri alipiga marufuku hiyo juzi wilayani hapa alipokuwa akipokea taarifa ya utekelezaji wa nyavu haramu zilizotumika kwenye shughuli za uvuvi katika maziwa hayo kwa kipindi cha mwaka wa fedha Julai 2022 hadi Juni, mwaka huu. Alisema wavuvi wanavua hadi vifaranga, jambo linalotishia uwepo wa samaki kwenye maziwa hayo.

Mulagiri alisema maziwa hayo ni muhimu katika kuiongezea pato Manispaa ya Singida, kutokana na shughuli za uvuvi, pamoja na kuwaingizia wananchi kipato cha kutosha katika kumudu maisha ya familia zao lakini pia lishe kutokana na samaki wanaovuliwa.

"Natoa agizo wavuvi kusitisha matumizi ya zana haramu katika shughuli za uvuvi na wananchi wasisite kuwaripoti wale wanaoendeleza hujuma kwenye maziwa haya ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria wafunguliwe mashtaka, badala ya kuteketeza tu zana zao pekee,"alisema.

Awali, Mkuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo, Dk. Adrianus Kalekezi, alisema kwa kipindi hicho zilikamatwa nyavu haramu ikiwamo kokoro sita, nyavu za matundu madogo 25 na nyavu aina ya Monofilament 17.



Meneja wa Kanda ya Kati wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joshua Ng'ondya (wa pili kushoto), akitoa elimu ya matumizi ya mbolea kwenye kilimo, kwa wananchi waliotembelea banda la TFRA katika maonyesho ya wakulima ya Nane Nane ya Kanda ya Kati, kwenye viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wazee wageuka ombaomba kwa kukosa uwezo, matibabu

**Na Mwandishi Wetu,**
CHEMBA

IMEELEZWA kuwa wazee wengi vijijini wasio na uwezo wamekuwa wakikosa matibabu na kulazimika kuombaomba.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Dorcas Aid International Tanzania limewakatia Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) zaidi ya wazee 160 wa kijiji cha Chambora wilayani Chemba ili kuondokana na adha hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wazee hao kwenye mafunzo ya haki kwa wazee yaliyotolewa na shirika hilo, Mwajuma Abdallah alisema shirika hilo limekuwa mkombozi kwao, kwa kuwa kabla ya kupatiwa msaada huo, walikabiliwa na adha ya kukosa matibabu kwa kuwa hawakuwa na fedha za kugharamikia huduma za afya.

"Tangu tupatiwe bima ya afya tumekuwa na uhakika wa kutibiwa tunapokwenda hospitalini, vituo vya afya na zahanati na afya zetu zimeimarika na zimekuwa bora zaidi," alisema Mwajuma.

Aliwaomba wadau mbalimbali kujitokeza kuungana na shirika hilo kusaidia makundi yenye mahitaji maalumu kuwa na uhakika wa matibabu.

Mwezeshaji wa Mafunzo ya Haki za Wazee, Wakili Mary Mwita, akitoa mada katika mafunzo hayo, alisema wazee wana haki sawa na makundi mengine na wanatakiwa kutetewa na kupata haki kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ubaguzi .

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Chemba, Efrazia Antony, alisema: "Shirika hili limefanya mambo mengi tangu mwaka jana. Kwa kuwa kuna miradi ya wazee na watoto imetekelezwa na limesaidiana na serikali kuleta maendeleo, hivyo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, nawapongeza. Pia natumia nafasi hii na kuwaomba wadau wengine kuiga mfano wa shirika la Dorcas."

Mratibu wa Mradi wa Wazee na Watoto kutoka Dorcas Aid International Tanzania na Tuwajali Development Initiatives, Goodluck Kivuyo, alisema wanahudumia wazee 160 na watoto 160 na kuwapa mradi wa kufuga kuku ili kuwawezesha kupata mahitaji ya msingi ya kila siku yakiwamo chakula na mavazi.

# Wakulima waipa tano TFRA udhibiti dhidi ya utapeli upatikanaji mbolea

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

WAKULIMA wamepongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kubuni mbinu ya kutoa namba ya siri itakayosaidia mkulima kupata mbolea ya ruzuku bila kikwazo kwenye msimu ujao wa kilimo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika maonyesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Kati yanayoendelea katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma, wakulima hao walisema hatua hiyo itadhibiti vitendo vya kitapeli vinavyofanywa na wajanja na hatimaye kuwaumiza wakulima.

Mmoja wa wakulima hao, Ibrahim Ndondole, alisema kitendo cha mkulima kupewa namba kimtasaidia kupata kwa urahisi mbolea ya ruzuku na kuondoa uchakuaji.

"Tunawashukuru sana TFRA kwa kubuni mbinu ya kutoa namba ya siri itakayomwezesha mkulima kupata mbolea ya ruzuku,tunaomba waendelee kubuni mbinu mbalimbali ili kuhakikisha uchakuaji wa mbolea unatoweka,"alisema Ndondole.

Alisema awali wakulima wengi walipata vikwazo wakati wa kujisajili na kupata mbolea hiyo.

Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati, Joshua Ng'ondya, alisema hivi sasa mamlaka hiyo imeweka mikakati ya kutumia vyama vya ushirika ili kupata mawakala ambao watafanya kazi kwa weledi.

Alisema wametoa elimu kwa zaidi ya mawakala 150 ambao watakaofanya kazi ya usambazaji mbolea ya ruzuku kwa wakulima mbalimbali nchini.

"Msimu huu TFRA imejipanga kuhakikisha hakuna malalamiko yoyote ya uchakajuaji mbolea na atakayebainika anafanya vitendo hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake," alisema.

Alitoa wito kwa wakulima kutoa taarifa TFRA pale wanapoona kuna uchakuaji wa mbolea unafanyika ili wahusika wachukuliwe hatua kali za kisheria.





# Waziri ataka kasi ujenzi wa nyumba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Makazi, Rahma Kassim Ali, amewataka makandarasi wanaojenga nyumba za biashara katika eneo la Mombasa Mjini Unguja kukamilisha kwa wakati ujenzi huo.

Akikagua ujenzi wa mradi huo jana, alisema nyumba hizo zinatakiwa kujengwa kwa viwango ili kuwavutia wanunuzi wanaohitaji na serikali kupata mapato.

Alisema matarajio ya nyumba hizo ni kukamilika kwa ujenzi Julai, mwakani, lakini serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Makazi, imemwomba mkandarasi anayejenga nyumba hizo kujenga nusu ya nyumba hizo na kuzikamilisha ifikapo Desemba, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Rahma, hivi sasa serikali imepanga kujenga nyumba zingine za bei nafuu kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar ambao wana kipato cha chini ili kupata makazi.

Alisema katika kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata makazi mazuri, wizara imejipanga katika kutatua changamoto za makandarasi wanaopewa nyumba za miradi ya maendeleo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC), Mwaisha Ali Said, alisema malengo ya ziara hiyo ni kuona ujenzi huo unavyoendelea kwa hatu ya awali ili kujua changamoto zilizopo na kufanyiwa kazi.

Alisema shirika limeridhishwa na hatua za ujenzi huo na litahakikisha linafanya ziara mara kwa mara kuona ujenzi huo unavyoendelea ili kukamilika kwa wakati.

Maneja Mradi kutoka kampuni ya Africab ambao ndio waliokabidhiwa ujenzi wa nyumba hizo, Anis Khatri, alisema kwa hatua za awali ujenzi huo unaendelea vizuri na hakuna changamoto iliyojitokeza, hivyo imani yake ni kwamba mradi utakamilika kwa wakati mwafaka.

Alisema serikali itarajie majengo mazuri na yenye viwango katika mradi huo na wajenzi wana uwezo mzuri katika kujenga majengo ya miradi mbalimbali.

# Bosi TARURA asifu mchango wanawake katika maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ,Mhandisi Victor Seff, amesema wanawake wana mchango mkubwa katika sekta mbalimbali za uongozi ikiwamo uhandisi na kuharakisha maendeleo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya kazi za wahandisi visiwani Zanzibar jana, alisema mchango wa wanawake katika sekta mbalimbali nchini hivi sasa ni mkubwa na msukumo maalumu unahitajika kuona kundi hilo linashiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa na kuleta maendeleo.

Alisema TARURA imejipanga kuhakikisha inaongeza nafasi za wahandisi wanawake kwa kuwajengea uwezo ili kushika nafasi za juu za uongozi katika idara mbalimbali za taasisi na kuleta ufanisi wa kazi.

Kwa sasa, alisema TARURA ina wahandisi 400 wanawake na wanafanya kazi katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na kwamba wote kwa ujumla wameonyesha ufanisi mzuri wa utekelezaji wa majukumu yao.

Hata hivyo, alisema idadi hiyo ni ndogo kutokana na wafanyakazi walioko katika taasisi hiyo ambayo ni zaidi ya 1,700. Kwa mantiki hiyo, wanawake katika taasisi hiyo ni asilimia 13. Alizitaja hatua zinazochukuliwa kwa sasa kuwa ni pamoja na kuwahamasisha na kuwapa moyo zaidi kujiendeleza katika kozi mbalimbali ili kwenda kufanya kazi na kuchukua nafasi katika maeneo mbalimbali ikiwamo mikoani.

Pia alisema bado nafasi nyingi za umeneja katika mikoa mbalimbali zinashikiliwa na wanaume na sasa wamejipanga vizuri kutoa msukumo unaostahili kwa wanawake.

"Wale ambao hawana sifa za uongozi tunahakikisha tunawapatia kozi fupi kwa ajili ya kuja kuchukua nafasi za uongozi katika ngazi ya umeneja wa mikoa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema TARURA inaendelea kutekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria ikiwamo kuzifanyia matengenezo barabara zilizoko vijijini ili kupitika na wananchi kufanya shughuli za maendeleo.

Alisema kwa kushirikiana na wadau katika ujenzi wa Barabara, TARURA imejenga barabara zenye urefu wa zaidi ya kilomita 144,000 zikijumuisha barabara za wilaya.

Katika maonyesho hayo, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akifuatana na viongozi wa serikali, alipata nafasi ya kutembelea banda la TARURA na kupata maelezo mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo.




Meneja Masoko na Mawasiliano wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Yesaya Mwakifulefule (kulia), akiwaelezea wanafunzi wa Sekondari ya Usongwe ya Mbalizi jijini Mbeya, jinsi mamlaka hiyo inavyofanya kazi, walipotembelea banda la TCAA katika maonyesho ya wakulima Nanenane kitaifa kwenye viwanja vya John Mwakangale jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kikwazo wanawake katika sayansi chatoweka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said, amesema kutokana na urithi wa imani kutoka kwa wahenga, jamii ilijengeka kifikra kuwa kuna kazi ambazo mtoto wa kike hapaswi kuzifanya ikiwamo kusoma masomo ya sayansi.

Zena aliyasema hayo katika sherehe za tuzo za wahandisi bora wanawake zilizofanyika juzi usiku wa visiwani Zanzibar.

Alisema jamii ilikuwa na imani hiyo ndiyo maana kwenye kada nyingi za sayansi zikiwamo uhandisi, nafasi nyingi zimeshikiliwa na wanaume ikilinganishwa na wanawake.

Hivi sasa, alisema imani hiyo imeanza kuondoka taratibu na sasa watoto wa kike wanasoma masomo ya sayansi na wameingia katika fani mbalimbali za kihandisi na zingine zinazofanana na hizo.

Kutokana na mabadiliko hayo, Mhandisi Zena aliwataka wanafunzi wa kike kujitokeza kuchangamkia fursa za masomo ya elimu ya juu katika uhandisi na sayansi ili kushiriki kikamilifu katika maendeleo na ujenzi wa taifa.

Serikali za Muungano na SMZ, alisema zinafanya kazi vizuri na wanawake ikiwamo katika kuwapatia fursa mbalimbali za kiuchumi kuingia katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Alisema bado hadi sasa wanawake waliosomea masomo ya uhandisi nchini ni kidogo sana na hivyo kushindwa kuzitumia fursa zinazopatikana katika maeneo hayo na hivyo kuchukuliwa na wanaume pekee.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikitoa motisha kila mwaka kwa wanafunzi wanaofaulu vizuri masomo ya sayansi kupata fursa za ufadhili wa masomo nchi za nje," alisema.

Alisema kuna uhitaji wa wanawake wengi zaidi kuingia katika masomo ya sayansi na uhandisi kwa sababu hivi sasa fursa ziko nyingi katika maeneo hayo pamoja na ajira.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Balozi Injinia Aisha Amour, alisema hivi sasa fursa nyingi za masomo katika kada ya uhandisi zinapatikana huku wanawake wakipewa kipaumbele cha kwanza.

Alisema katika Wizara ya Nishati kuna nafasi za ufadhili wa masomo katika masuala ya nishati endelevu ambazo zimetengwa kwa wanawake pekee.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Wahandisi Wanawake Tanzania (TAWECE), Rihanna Juma, alisema wakati umefika sasa kuondokana na mawazo yanayotokana na mfumo dume kwamba kazi za uhandisi zinawahusu wanaume pekee.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT



**STELLA URAFIKI GANI WA MASHAKA?** Ukurasa.14

JUMAMOSI AGOSTI 5, 2023



# KUMECHAFUKA

MWEZI Julai ilikuwa kama bahari ilichafuka, kama kuna mtu ni mdau wa muziki wa Bongo Fleva, hakuna aliyetulia kutokana na muda wote kuwa makini na kinachojiri kutoka kwa wasanii wakubwa walionekana kutoana povu.

Unaweza kusema ni mwezi ulioshuhudia vurugu nyingi na kusababisha tasnia ya muziki kutikisika baada ya wasanii hao mastaa Diamond Platnumz, Ali Kiba na Harmonize kuwa katika malumbano makubwa.

Kitendo cha Ali Kiba kumshauri Diamond kuwa makini kutokana na tuhuma zinazomuandama za kuiba nyimbo, imezusha zahama kubwa kiasi ambacho wawili hao walianza kupeana maneno makali na yenye kuhudhi hadharani.

Ugomvi huo uliteka vichwa vya habari za udaku, huku Diamond alionekana ndiye aliyekasirika zaidi, kila mara alionekana akituma ujumbe katika ukurasa wa instagram akimuonya Ali kiba kwamba akitoa nyimbo zake aache kumfuata fuata kwani hamfikii kimapato.

Kama haitoshi, Diamond alimuita Ali kiba jina la malkia badala ya mfalme na kwenda mbali kwa kumtaka aache kujiita mwenye sauti nzuri ya kuimba, badala yake yeye ni mbana pua tu.

Wakati watu wanahangaika na ugomvi wa mafahari hao wawili, mwanamuziki mwingine Harmonize, aliibuka na zahama nyingine baada ya kuamua kutoa siri ya maisha yake na aliyekuwa mpenzi wake Kajala Masanja.

Harmonize na Kajala walirushiana maneno makali kutokana na msanii huyo kutoa wimbo wake mpya unaoitwa Dear Ex, ambao ndani yake ametoa siri jinsi Kajala na binti yake Masanja walivyomtenda.

Katika wimbo huo, Harmonize anaweka wazi jinsi Kajala na binti yake walivyomuhangaisha kifedha na kumuacha hoi wakidhani tayari wamemuangamiza kiuchumi.

BASI SAWA

## Billnas mbona watu walishasahau



RAPA anayetamba kuwa katika ndoa imara, William Nicholaus Lyimo, maarufu kama Bill Nass, amewataka watu kuacha kumchonganisha na mwanamitindo Hamisa Mobetto.

Kwa muda mrefu, watu wamekuwa wakihusisha mtoto wa pili wa mwanamitindo huyo Dylan kuwa baba yake ni Bill Nass na kukazia hoja hiyo kuwa eti wanafanana.

"Sijui nia yao au dhumuni la hiyo habari ilianzia wapi lakini mimi mtoto hanihusu kwa namna moja au nyingine. Wakati ambao tulifahamiana naye, tayari alikuwa na watoto wake wawili. Kwa mara ya kwanza namuona alikuwa na watoto. Kutokea hapo sijawahi kuwa na jamb lolotee," alisema Bill Nass.

## Risandi aomba 'Baraka za Mungu'



MWIMBAJI wa Injili, Risandi Laizer amewashukuru mashabiki kwa kuupokea vizuri wimbo wake mpya unaoitwa Baraka za Mungu.

Akiuzungumzia wimbo huo, Laizer, amesema wimbo huo uko tofauti na ndio maana mapokezi yamekuwa ya kushangaza.

"Huu ni mwendelezo mzuri wa kuhakikisha sipotei tena kwenye huduma hii ya uimbaji, Baraka za Mungu ni wimbo uliogusa maisha ya wengi ndio maana mapokezi yamekuwa makubwa tofauti na nilivyotegemea," amesema Risandi.



## Harmonize utakikwepaje Kiswahili?

WIMBO mpya wa msanii pendwa wa Bongo Fleva, Harmonize, umeibua mjadala mkali baada ya mwanamuziki huyo kuonekana amekiuka kauli yake ya kuacha kuimba kwa lugha ya Kiswahili.

Kibao hicho 'Tena' alikiachia wiki hii ambacho amekiimba kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza, ametoa baada ya kutoa kauli kuwa album ya HIGH SCHOOL ilikuwa ya mwisho kwa yeye kuimba tena nyimbo zake kwa lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, kilichowashangaza mashabiki zake ni kwanini msanii huyo kaamua kurudi tena katika lugha yake mama ikiwa yeye aliapa kutotumia katika kazi zake.



## Kajala yafichue yote

AMA kweli bahati haiji mara mbili! Eti mwanadada mrembo Kajala Masanja ni sawa na kuacha mgodi wa fedha kwa Harmonize, kutokana na msanii kumkabidhi kila kitu ikiwamo namba za siri za kadi za benki wakati wakiwa katika uhusiano wa kimapenzi.

Siri hiyo nzito imeibuliwa na Harmonize mwenyewe baada ya kubainisha kwamba licha ya kumpa namba za siri, pia alikuwa akichukua asilimia 10 ya mapato yake yote.

Mkali huyo wa 'Single Again' ameendelea kuwa alimtaka Kajala wakati akisimulia maisha yao ya zamani na asisahau kuwaambia suala hilo.

## Miduara mi 5 konki ya Babu Njenje

**Na Adam Fungamwango**

NI mwaka wa tatu huu umepita tangu, anga la muziki wa Tanzania kugubikwa na wingu zito kwa kuondokewa na mwanamuziki mkongwe Mabrouk Hamisi Omari maarufu kama 'Babu Njenje.'

Ni mwanamuziki aliyejizolea umaarufu mkubwa kwenye fani hiyo, hasa kwenye aina yake ya uimbaji wa nyimbo za mduara.

Babu Njenje aliyekuwa mwimbaji kiongozi wa bendi ya Kilimanjaro Revolution alifariki dunia jijini Dar es Salaam, Mei 4 mwaka 2020 na kuzikwa siku hiyo hiyo kwenye makaburi ya Kisutu jijini Dar es Salaam.

Ndiye mwanzilishi wa miziki ya mwambao aina ya mduara ambayo baadaye ilikuja kuboreshwa na kutiwa chumvi na mkali mwingine wa miziki ya aina hiyo na mmiliki wa bendi ya Chuchu Sound, Yussuf Ahmed Alley, maarufu kama Bwan' Chuchu ambaye alifariki dunia 2010.

Hizi ni baadhi ya nyimbo ambazo zilimfanya Babu Njenje kutamba na kupata umaarufu sana miaka ya '90 hadi mwanzoni mwa mwaka 2000.

**Njenje**

Huu wimbo ulitoka katikati ya miaka ya '90, na ndiyo ulioitambulisha bendi hiyo na kupata umaarufu mkubwa.

Mbali na hilo, umaarufu wa wimbo huu, ndiyo uliifanya bendi kuitwa jina la 'Wana Njenje', lakini pia muimbaji kiongozi marehemu, kupachikwa jina la 'Babu Njenje' pia.

"Njenje oo Njenje na kiparamoto Njenje. Kitamutamu cha boga, kutia nazi kunoga, mkono wataka kula, maungo yaona woga." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye kibao hicho, ulioimbwa na mtindo wa mduara.

**Kinyaunyau**

Kuonyesha kuwa hawakubahatisha, Babu Njenje na bendi yake ya Kilimanjaro walirudi na wimbo mwingine ambao nao ulitamba sana waliouita 'Kinyaunyau.' Nao pia upo kwenye mahadhi ya mduara ambao ulizidi kumpa sifa.

"Kinyaunyau kikia cha pweza, mwataka mambo hamtayaweza." Ni sauti ya Babu Njenje ikihanikiza kwenye wimbo huo.

**Kachiri**

Mashabiki wa Babu Njenje na bendi hiyo walizidi kujipatia uhondo baada ya bendi hiyo kuibuka tena na kibao kingine kitamu kiitwacho 'Kachiri.'

Kama kawaida ni mtindo wa mduara ambao uliwachetua mashabiki wengi ambao wanajipanga foleni na kukaa mduara, huku mwenyewe akihanikiza mwishoni na kibwagizo kilichobeba zaidi wimbo huo.

"Kachiri Kachiri saga, mume wangu kasafiri, kaniachia kigoma na mtindo wa hariri, kaniachia korola na madola teletele, na kidani cha dhahabu na kiatu cha kokokoko, kisimu cha mkononi,

Buzi langu limo ndani nimelifunga kiguzoni, mchunaji una nini? katafute Vingunguti, buzi langu hulipati, Kachiri saga, Kachiri saga, Kachiri saga."

**Nchecheme**

Babu Njenje na Kilimanjaro Band walikuwa hawabahatishi. Yeyote aliyedhani walikwisha alikosea.

Baadaye wakatoka na ngoma nyingine waliyoiita 'Nchecheme' ambayo kama kawaida ilikuwa kwenye mahadhi ya mduara, iliyozidi kuwapa heshima na umaarufu

'Mama mwanangu leo, ukawacha napinda mgongo mie, kwani sina neno." maneno hayo yamo kwenye wimbo huo.

**Ndembele**

Ni wimbo ambao pia uliimbwa na Babu Njenje, lakini huu ulikuwa tofauti kidogo kwani uliimbwa kwenye lugha ya Kisukuma mchanganyiko na Kinyamwezi, ingawa mipigo haikutofautiana sana na mduara.





## Mwachumvi: Giza likizidi kunakaribia kucha

**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wana msemo mmoja unaosema kuwa 'mgaagaa na upwa hali wali mkavu.'

Tafsiri yake kwa kiswahili kinachoeleweka vizuri ni kwamba mtu anayezungukazunguka pwani ya bahari, basi huwa hakosi kitoweo.

Tukirudi kwenye maana na ni kwamba mtu yeyote anayetoka kwenda kutafuta huwa hakosi chochote, ni tofauti na mtu anayekaa tu nyumbani. Hii inafana na ile ya 'mtembea bure si sawa na mkaa bure'.

Hali kama hii inajitokeza kwenye filamu ya 'Mwachumvi.' Wahusika kwenye filamu hii ni Ali Kalawi, Haji Mboto, Luckey Lukamo, hayati King Majuto, Muhogo Mchungu, Anita Sudi, Mau Chiwaga, Sabrina Paul na wengineo.

Anaanza kuonekana Mzee Majuto na kijana wake Kalawi wakizungumza. Majuto anampa siri mwanaye kuwa hana uhakika na binti yake Mwachumvi kama ni mtoto wake kweli au amebambikiwa.

Anamwambia Kalawi kuwa wakati akiwa mdogo, alikuwa na uhusiano na mwanamke mmoja kijiji cha jirani. Lakini baadaye akawa mjamzito. Huko huko kijiji jirani alikuwa na bwana mwingine, hivyo alipoambiwa akaukataa ujauzito.

Alipojifungua, binti huyo alikuja kumbwagia mtoto akiwa bado mdogo na yeye kutokomea kusikojulikana. Akasema ilileta ugomvi kwa mama yake Kalawi, lakini baadaye akakubali kumlea, hadi mama alipofariki.

Akamtaka kijana wake asimwambie lolote dada yake kuhusu jambo hilo, hajui chochote, anachofahamu marehemu mama Kalawi ndiyo mama yake mzazi.

Kalawi akamuahidi baba yake kuwa hatofanya hivyo. Pamoja na hayo, Majuto alionekana kumtenga Mwachumvi kimasomo kwa sababu hakumpeleka shule.

Kijijini hali ya maisha inakuwa mbaya, Kalawi na Mwamchumvi wanatoroka.

Dar kama kawaida ikawapokea. Chumba kimoja nyumba ya kupanga ikawa ndiyo makazi yao.

Aina yake ya maisha ya kulala chumba kimoja mtu na kaka yake ilisababisha watu wawafikirie vibaya. Walichokila na kukivaa wanakijua wenyewe.

Misukosuko wanayoipata, wanampigia simu baba yao Majuto kuomba walau auze kipande cha shamba na kuwatumia pesa. Majuto alikataa kwa sababu walimtoroka.

Kalawi akawa anafanya kazi ya kusafisha magari. Moja yagari lilikuwa la Mboto, kijana aliyekuwa ana kazi na kipato kizuri. Kalawi anamhadithia maisha yake jinsi yalivyo. Haji anaingiwa na huruma na kwenda kuangalia wanapoishi. Anamkuta binti mmoja mrembo Mwachumvi. Mate yakamvuja.



# Stella urafiki gani wa mashaka?

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Stella Damasus, amezungumza kuhusu kuanguka kwa ndoa yake ya tatu, akisema bado ana urafiki na mke wa kwanza wa mume wake wa zamani.

Akizungumza katika podikasti na mchekeshaji maarufu Teju Babyface, Stella alifafanua kuwa, kinyume na imani ya wengi unapoondoka kila kitu kinakwisha, yeye ni rafiki na mke mwenzake wa zamani, Doris Simeon.

"Ni mwanamke mwenye akili, mrembo, ana kipaji kikubwa. Mionekano ya nje ni kama kichaa, mtu niliyemfahamu hata kwa njia ya simu alikuwa tofauti kabisa ni rafiki yangu," amesema.



## Wizkid azidi kupaa

STAA wa muziki wa Nigeria, Wizkid amevunja rekodi baada ya kufanikiwa kuujaza uwanja wa Tottenham, nchini Uingereza.

Katika tamasha lake lililofanyika Julai 29, zaidi ya watu 60,000 walijitokeza kumtazama mshindi huyo wa Grammy katika onyesho lake hilo.

Onyesho hilo ni moja wapo ya vituo vya ziara ya mwanamuziki huyo yenye lengo la kutangaza albamu yake ya tano ya 'More Love, Less Ego' ambayo aliiachia Novemba 2022.

## Angus aaga dunia

MWIGIZAJI maarufu wa Marekani Angus Cloud amefariki dunia.

Msanii huyo anayefahamika kama Neill katika mchezo wa kuigiza unaopendwa na vijana, aliaga dunia Jumatatu, nyumbani kwao Oakland, katika jimbo la California.

Kulingana na TMZ, familia yake iliripoti kwamba kabla ya mauti kumfika, Cloud alikuwa na tatizo la msongo wa mawazo kutokana na kifo cha baba yake, ambaye alizikwa nchini Ireland wiki iliyopita.

Wanaripoti kuwa mama wa mwigizaji huyo alipiga simu ya dharula akiripoti mtoto wake kazidiwa na alipofikishwa hospitali ilibainika tayari amefariki.





## Kanye West arudishwa X

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West imerudishwa katika mtandao wa Twitter ambao sasa unafahamika X baada ya kufungiwa mwaka jana.

Rapper huyo alifungiwa akaunti yake kutokana na ukiukaji wa sera za kampuni hiyo mara nyingi kwa matumizi ya maneno yenye utata.

West alikuwa nje kwa muda wa miezi saba baada ya kutoka kauli za uchochezi dhidi ya Wayahudi mnamo Desemba 2023.

## Drake ajipambanua yeye mwamba

MSANII wa muziki raia wa Canada, Drake ndiye rapa wa kwanza katika historia ya Marekani kulipwa zaidi ya dola milioni 5, kwa kupanda jukwaani.

Kulingana na tweet ya mwandishi wa box score, mwanamuziki huyo mwenye umri wa miaka 36 alijikusanyia dola milioni 5.032 kila usiku kwenye Ukumbi wa Capital One Arena mjini Washington, D.C.

Kitita hicho cha pesa alijipatia, kuanzia Julai 28 mpaka 29 katika ziara yake na 21 Savage.



# Uwekezaji kiwanda wamkuna Waziri

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, ameridhishwa na uwekezaji wa kiwanda kipya cha kwanza Tanzania cha kuunganisha vishikwambi na vifaa vya mawasiliano cha Tanztech Electronics Limited kitakachosaidia kuimarisha teknolojia ya mawasiliano.

Dk. Kijaji alieleza kuridhishwa na uwekezaji huo juzi alipotembelea kiwanda hicho, kilichoko Njiro jijini Arusha, akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani hapa.

Alisema ameridhishwa na uwekezaji huo kwa kuwa ni hatua mojawapo ya kutatua tatizo la upungufu wa vishikwambi katika shule za awali na sekondari.

"Niwapongeze sana kwa uwekezaji huu. Nina imani vishikwambi mtakavyozalisha vitasaidia shuleni kwa kufundishia wanafunzi namna bora ya kutumia teknolojia ya mawasiliano pamoja na kujifunza mitaala mbalimbali,"alisema.

Waziri alisema ndoto ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuwapo kwa fursa za uwekezaji katika sekta ya sayansi na teknolojia inakuwa kwa kasi na kupiga hatua ili kuleta maendeleo kwa Watanzania kuendana na dunia ya kidigitali.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzteck Eletronics Limited, Gurveer Hans, kuboresha huduma zake na kuanza kuzalisha bidhaa zinazokwenda na wakati katika soko la teknolojia ya sayansi.

Alisema vishikwambi vitakavyozalishwa visaidie kukidhi mahitaji ya elimu kwa wanafunzi, pia vitatumika kwenye ofisi na asasi mbalimbali katika jamii.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema serikali iko tayari kusaidia kufikia malengo ya uzalishaji wa vishikwambi na vifaa vingine vya mawasiliano kama dira yao inavyoelekeza.

"Serikali imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji na imetoa fursa kwa wawekezaji kuja nchini kuwekeza na tuko tayari kushirikiana na mwekezaji yeyote kuhakikisha kwamba uwekezaji unakua wa tija na mafanikio kwa taifa,"aliongeza Waziri Kijaji. Naye Hans alisema kiwanda hicho,kimeanzishwa kwa ushirikiano na watu wa China ambao wana uzoefu mkubwa kwenye masuala ya teknolojia.

Mkurugenzi huyo alisema kiwanda hicho kwa sasa kina uwezo wa kuunganisha simu janja 40 kwa mwezi, vishikwambi 30,000, kompyuta mpakato 15,000 na 'smart projectors' 10,000.

Vilevile alisema matarajio ya kiwanda ni kuongeza teknolojia za kisasa nchini kwenye masuala ya kidigitali kwa kuwa watashirikiana na serikali katika kusambaza vishikwambi shuleni kwa gharama nafuu.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali mpya ya wilaya ya Muheza ya Samia Suluhu, Gerard Kazumba (kulia), alipofanya ziara ya kukagua majengo ya hospitali katika kijiji cha Lusanga, wilayani humo mapema wiki hii. Wengine ni Katibu wa CCM wilaya hiyo, Simoni Leng'ese (wa pili kulia), Katibu Tawala wilaya hiyo, Mohamed Mfaki (wa tatu kulia) na (kushoto) ni Katibu wa CCM mkoa huo, Selemani Mzee Selemani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mchimbaji madini asisitiza utunzaji ardhi

**Na Woinde Shizza,** LONGIDO

WANANCHI wa Kijiji cha Elesin'geta Kata ya Mundarara, Longido mkoani Arusha, wamesisitizwa kuhifadhi na kutunza ardhi wanayoimiliki kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Kadhalika vijana wa vijiji hivyo, wametakiwa kufanya kazi kwa bidii na kutumia fedha wanazopata kuzielekeza kwenye shughuli za maendeleo na kujikwamua kiuchumi badala ya kuzitumia kwenye anasa.

Rai hiyo, ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Kampuni ya Uchimbaji wa Madini ya Rubby ya Sendeu Mining Limited, Gabriel Laizer, wakati akizungumza kwenye hafla ya kumsimika Mwenyekiti mstaafu wa Kijiji cha Elesin'geta,

Akwelino Nikeni, kuwa chifu wa ukoo wa Kipuyo (Laigwanani).

Mkurugenzi huyo alimpongeza kiongozi huyo mstaafu kwa kazi nzuri aliyofanya wakati wa uongozi wake kwa kuwa aliwasaidia wananchi wa kijiji hicho, kupata maeneo ya kuchimba madini ya rubi.

Alisema kuna haja kwa wananchi wa Longido kuendelea na jitihada za kulinda na kuhifadhi ardhi kwa ajili ya vizazi vijavyo na endapo wataitumia vibaya, itasababisha watoto watakaozaliwa baadaye kukosa ardhi.

"Na kwa vijana mlioko hapa, mnaofanya shughuli mbalimbali ikiwamo ya uchimbaji wa madini, tumieni vizuri fedha mnazopata kwa kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo na si kwenye kufanya anasa kwa kuwa mkiwekeza itawasaidia nyie wenyewe na vizazi vyenu pamoja kuongeza pato la taifa," alisema Laizer.

Pia alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia wananchi wa wilaya hiyo maeneo kwa ajili ya kuchimba madini hayo, kwa kuwa yamewapatia ajira vijana wengi na kuwaondokana na umaskini.

"Pia namshukuru Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, kwa kuwa wamesaidia wananchi kupewa maeneo haya kwa ajili ya kufanya uchimbaji," alisema.

Katika hatua nyingine, Sendeu kwa kutambua mchango wa mwenyekiti mstaafu wa kijiji hicho, alimkabidhi nyumba aliyomjengea pamoja na gari aina ya Toyota Noah kama shukrani.

Naye Nikeni aliwashukuru wananchi kwa namna walivyotambua mchango wake kusaidia jamii kipindi cha uongozi wake, hivyo aliwahaidi kuwa ataendelea kuwapa ushirikiano hata kipindi ambacho hayuko katika uongozi.

"Namshukuru Laizer kwa kunipa gari hili, nina ahidi gari nililopewa mbali na matumizi yangu binafsi, pia litatumika kuwasaidia wananchi wa kijiji hiki na kata wakiwa na uhitaji nalo na nyumba hii itanisaidia kuishi mimi na familia yangu," alisema Nikeni.

# DED aagizwa shule Siha One kufunguliwa

**Na Anjela Mhando,** SIHA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Siha, limemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kuhakikisha ifikapo Jumatatu ijayo, Shule ya Sekondari Siha One, iwe imefungiliwa ili wanafunzi waendelee na masomo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Duncan Urassa, alitoa agizo hilo katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo.

Kikao hicho kilikuwa na ajenda ya uwasilishaji wa taarifa za maendeleo ya kata kwa kipindi cha robo ya nne kuanzi Aprili hadi Juni, mwaka huu.

Diwani wa Biriri, Frank Kisinani, alihoji ni lini shule hiyo itafunguliwa na wanafunzi waanze kupata masomo ili kuepuka adha ya wanafunzi katika kata hiyo kutembea umbali mrefu kufuata elimu katika kata za jirani.

"Shule ya Sekondari Siha One usajili wake umekamilika na halmashauri yetu ilipata kutoka serikali kuu Sh. milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo na tayari majengo yamekamilika yakiwamo vyumba vya madarasa, maabara na vyoo. "Naagiza ifikapo Agosti 7, mwaka huu, wanafunzi waanze masomo katika shule hiyo. Naelekeza ofisi ya mkurugenzi kuhakikisha wanakwenda kuazima meza na madawati kwenye shule za sekondari zilizo na ziada ya vifaa na kuvipeleka katika shule hiyo wanafunzi waendelee na masomo," alisema Urassa.

Awali, Diwani Kisinani alisema shule hiyo ilishindikana kufunguliwa kutokana na kukosekana kwa madawati na meza, hivyo aliiomba serikali kusaidia kununuliwa kwa vifaa hivyo ili wanafunzi waendelee na masomo.

Kaimu Ofisa Elimu Sekondari, Herman Msasa, alisema changamoto ya mfumo wa kifedha kufungwa mwisho wa mwaka wa bajeti, ilisababisha kushindikana kupatikana kwa fedha kwa ajili ya kununua vifaa hivyo. Aidha, alisema idara ya elimu tayari imefanya jitihada ya kutafuta utaratibu wa kutatua changamoto hiyo ikiwamo kupita kwenye shule za sekondari zenye ziada ya madawati na meza na kuazima.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Kusikiliza redio enzi hizo hadi baba arudi nyumbani

## -Watoto huchaguliwa vipindi vya kusikiliza

**Na Adam Fungamwango**

SIKU hizi mtoto anaingia ndani, anamkuta baba yake anaangalia televisheni. Iwe anaangaalia mpira, taarifa ya habari au hata tamthiliya, anakwenda hadi mbele yake. Anaweza kumsalimia akitaka au hata asimsalimie, atachukua rimoti nakubadilisha kwasababu anataka kuangalia katuni.

Baba anaweza kutaka kuweka ngumu, lakini anazidiwa na mtoto. Anaweza kuweka katuni au kitu chochote anachotaka kuangalia kwa wakati huo, inawezekana ikawa hata tamthiliya anayoitaka yeye.

Mzee atapigwa na maneno ya 'dadidadi' ya uongo na kweli, atasimama na kuvaa shati lake, huyooo anaondoka.

Kama mpira anaweza kwenda kuangalia kibandaumiza, au kuamua tu kwenda sehemu yoyote kutembea, lakini haiondoi ukweli kwamba amenyanyuliwa na kukatishwa kuangalia televisheni na mtoto au watoto wake.

Atakuwa ana gugumia tu njiani "watoto wa siku hizi bwana." Hayo ndiyo maisha ya wazazi wengi na watoto zao kwa sasa.

Wazazi na watoto zao siku hizi wamekuwa wanaishi kama marafiki fulani hivi. Yaani mtoto anakuwa na haki unaweza ukadhani ana ubia na baba yake.

Kuna maisha ya kudeka kwa wazazi kwa watoto wengi wa kisasa kuliko wa zamani. Ukiangalia zamani hata mtoto alikuwa ni wa jamii nzima na sio wa mzazi peke yake.

Mtoto 'akizingua' mtaani ataadhibiwa na yeyote yule ambaye ni mtu mzima, huku akitishia kuwa atakwenda kumwambia mzazi wake.

Mtoto mwenyewe hatakama akiadhibiwa hathubutu kwenda kusema kwao. Kwasababu inaweza kusababisha kesi kuanza upya.

Mzazi ataanza kujiuliza kwanini mzee fulani kampiga na atataka kujua ukweli wa jambo hilo. Ikibainika kuwa alipigwa kwasababu alikutwa anafanya kosa fulani njiani, atapigwa tena.

Hii ilisababisha watoto wa zamani wakiadhibiwa mtaani na mzee wa makamu kwasababu ya makosa ya kimaadili hathubutu kwenda kusema kwao. Yanabaki hukohuko.

Siku hizi mambo yamebadilika. Ukimpiga mtoto hivi, unaweza kujiwa na ukoo mzima 'kukuchamba.' Utasutwa mpaka ukome. "Kazae wako ndiyo umpigepige kama ngoma."

Sasa aliyempiga awe mwanamke na hana mtoto ndiyo atakoma.

Kila mmoja kwa sasa analea mtoto wake tu. Mtu mzima akimkuta mtoto njiani anafanya kitu chochote hana ubavu wa kumfanya lolote. Anaogopa.

Ukaribu wa wazazi kwa watoto wao kwa miaka ya sasa yana faida na hasara zake na hata uleaji wa wazazi wa zamani ambapo watoto walikuwa kama wapo kwenye kambi ya jeshi ulikuwa na faida na hasara zake pia.

Wazazi wa zamani walikuwa hawamnyimi mtoto viboko. Kosa la kujirudiarudia, liliweza kusababisha kucharazwa bakora kila siku.

Wakati watoto wa sasa wanakaa sebuleni wakiwa wana uhuru wa kuchagua chaneli yoyote ya televisheni na kuangalia hata wazazi wao wakiwepo, zamani haikuwa hivyo.

Kwanza hakukuwa na televisheni na hata miaka ambayo televisheni zilianza kuingia nchini, bado kuangalia ilikuwa mpaka mzazi awepo.

Hebu turudi nyuma miaka ambayo televisheni hazikuwepo.

Redio yenyewe kusikiliza hadi baba awepo.

Kitendo chochote cha kutafuta redio ilipo na kuifungulia mwenyewe hayupo, ni kosa kubwa ambalo linaweza kusababisha adhabu ya viboko.

Halafu walikuwa na uwezo wakuweka sehemu ambayo hataukiishika tu na kuifungulia, ukairudisha tena akirudi anajua kuwa kuna mtu ameigusa redio yake.

Na hadi mtasema ni nani.




Yeyote anayetaka kusikiliza redio ni lazima amsubiri baba arudi, afungilie ndipo watoto mkae msikilize. Na hata kusikiliza kwenyewe si vipindi vyote. Kuna vipindi ambavyo watoto wanaambiwa waondoke kwani haviwahusu.

Wapo watoto waliokuwa watundu zaidi ambao walikuwa na uwezo wa kufungua, kusikiliza na kurudisha bila baba kujua.

Hapo sasa kuna kuzidiana akili, kati ya baba na mtoto. Ukimkuta baba mwingine akiona betri zinaisha wakati hajatumia kwa muda mrefu, anaanza kuhisi kuna mtu huwa anafungulia redio yake.

Atakachofanya nikuzigeuza betri. Kama redio ni ya betri nne, ya katikati itageuzwa ielekee upande mwingine, hivyo yeyote atayeifungua itaendelea kunyamaza tu. Ni udadisi wa hali ya juu tu ndiyo unaweza kugundua kuwa betri moja limegeuzwa, vinginevyo unaiacha na kuendelea na shughuli zako.

Hii haikuwa na maana kuwa wazazi wa zamani walikuwa na roho mbaya na hawapendi watoto wao, la hasha.

Ilikuwa ni kuwa jenga kwenye utamaduni wa nidhamu na adabu.

Pia ikumbukwe kipindi hicho waliokuwa na redio ni wachache, na sio wengi waliokuwa na uwezo wa kuimiliki.

Kwasababu hiyo ilikuwa ni kama kuilinda ili watoto wasiharibu. Hata upatikanaji wa betri nao ulikuwa ni wa mbinde. Unaweza kuwa na redio, lakini usiweze kupata betri hata miezi miwili. Baba akaishia tu kubondabonda betri zilizopo na kuzianika juani, ili redio ipate kuongea hata kwa dakika 30 tu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Ukraine yashambulia meli ya Russia

KYIV, Ukraine

MELI ya kijeshi ya Russia, imeharibiwa baada ya kushambuliwa na ndege isiyo na rubani ya jeshi la Ukraine katika Bahari Nyeusi.

Shambulio hilo limeripotiwa kutokea karibu na bandari ya Russia ya Novorossiysk, ambayo ni kitovu cha usafirishaji wa bidhaa za nchi hiyo.

Wizara ya ulinzi ya Russia, ilisema imezima shambulio la Ukraine kwenye kambi yake ya jeshi la wanamaji lililohusisha ndege mbili zisizo na rubani za baharini.

Hata hivyo, haikukiri kuwa kulikuwa na uharibifu wowote.

Lakini vyanzo vya usalama vya Ukraine, vilisema kuwa meli hiyo inayoitwa Olenegorsky Gornyak ilipigwa na kuharibiwa vibaya.

Waliiambia BBC kuwa ndege isiyo na rubani ilikuwa imebeba kilo 450 za baruti iliigonga meli hiyo.

Russia haikutaja uharibifu wowote katika ripoti yake ya tukio hilo.

Ndege zisizo na rubani za baharini ni vyombo vidogo visivyo na rubani vinavyofanya kazi juu au chini ya uso wa maji.

Video iliyotumwa kwa BBC na chanzo cha idara ya usalama ya Ukraine, ilionyesha ndege hiyo isiyo na rubani ikikaribia meli inayodhaniwa kuwa ni Olenegorsky Gornyak.

Picha hiyo ilionyesha jinsi ndege hiyo ikisafiri kabla ya picha kukatika, na kuashiria ilitokana na kugongana.

Video nyingine ambayo haijathibitishwa inadhaniwa kuonyesha meli hiyo upande mmoja.

Olenegorsky Gornyak ni meli , iliyoundwa kwa ajili ya kuzindua vikosi vya amphibious vilivyopo karibu na ufuo lakini pia hutia nanga na kupakua mizigo haraka bandarini.

Uharibifu wowote uliofanywa unaweza kuathiri juhudi za Russia za kurudisha nyuma vikosi vinavyopigana katika eneo la kusini mwa Ukraine.

Bandari ya Novorossiysk ilisimamisha shughuli zake kwa muda kufuatia shambulio hilo, kulingana na Caspian Pipeline Consortium, kampuni ambayo ambayo hupakia mafuta kwenye meli za mafuta kwenye bandari hiyo.

**BBC**

# Trump apandishwa kizimbani atuhumiwa kutengua matokeo

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani Donald Trump, amekana mashtaka ya kula njama ya kutengua uchaguzi wa 2020.

Kesi hiyo imeanza kusikilizwa jana katika mahakama ya ya shirikisho mjini Washington DC.

Kesi ambayo ilichukuwa muda mfupi, Trump alizungumza kwa upole ili kuthibitishia mahakama kuwa hana hatia.

Baada ya kutoka nje ya mahakama aliwaambia waandishi wa habari kuwa kesi hiyo ilikuwa mateso kwa mpinzani wa kisiasa.

Rais huyo wa zamani alionekana kwa mara ya tatu ndani ya miezi minne akipanda kizimbani kwa makosa ya uhalifu.

Trump aliingia kupitia mlango wa nyuma wa mahakama hiyo ambayo iko katikati mwa mji mkuu huo, jirani na eneo ilikotokea ghasia la majengo ya bunge la Marekani.

Hakimu Moxila Upadhyaya, alimwambia rais huyo wa zamani asiwasiliane na watu kuhusu kesi hiyo na kumuonya asipotii agizo hilo hati ya kukamatwa kwake itatolewa na dhamana yake itabatilishwa.

Waendesha mashtaka waliomba kesi hiyo kusikilizwa kwa haraka.

Lakini wakili wa Trump John Lauro alisema watahitaji muda zaidi kujiandaa.

Alisema muda waliotumia upande wa mashtaka ulikuwa wa kushangaza kutokana na kwamba uchunguzi wenyewe umechukua miaka mitatu.

Mashtaka hayo yaliyowekwa hadharani siku ya Jumanne ni kula njama ya kudhoofisha, kuzuia, na kuvuruga shughuli za serikali kwa kutumia ulaghai na udanganyifu.

Trump alishindwa katika uchaguzi wa 2020 na mpinzani wake wa chama cha Democratic, Joe Biden, lakini alikataa kukubali matokeo.

**BBC**



Watoto wakipita katika magari yaliyoteketezwa baada ya kuibuka mapigano kati ya jeshi na wanamgambo katika eneo la Amhara. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Ethiopia yatangaza hali ya hatari eneo la Amhara

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

SERIKALI ya shirikisho nchini Ethiopia imetangaza hali ya dharura kufuatia siku kadhaa za mapigano kati ya jeshi na wanamgambo katika eneo la Amhara.

Mapigano hayo yaliyozuka katika eneo hilo la pili kwa ukubwa nchini humo kati ya wanamgambo wa Fano na wanajeshi wa Ethiopia na kugeuka kuwa mgogoro unaohatarisha usalama.

Juzi, serikali ya Amhara iliomba msaada zaidi kutoka kwa mamlaka ya shirikisho ili kurejesha hali ya utulivu.

Hata hivyo, taarifa ya ofisi ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed ilitangaza hali ya dharura, lakini haikubainisha iwapo hatua hiyo itatekelezwa katika mkoa wa Amhara pekee au nchini kote.

**DW**

# Rais aliyepinduliwa aiomba Marekani kumrejesha

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS aliyepinduliwa wa Niger, Mohamed Bazoum, ameiomba Marekani na jumuiya ya kimataifa kusaidia kumrejesha madarakani.

Katika ombi hilo, Bazoum alisema nchi hizo zisaidie kurejesha utaratibu wa kikatiba ambao umefutwa baada ya mapinduzi hayo yaliyofanyika wiki iliyopita.

Katika maoni yake yaliyochapishwa kwenye gazeti la Washington Post, Rais Bazoum alisema alikuwa akiandika ujumbe huo katika hali ya mateka.

Machafuko yameibuka katika taifa hilo la Afrika Magharibi tangu alipoondolewa madarakani. Siku ya Alhamisi, viongozi hao wa mapinduzi walitangaza kuwa wanawaondoa mabalozi wa nchi hiyo kutoka Ufaransa, Marekani, Nigeria na Togo.

Katika taarifa iliyosomwa kwenye televisheni ya taifa, walisema kazi za mabalozi wanne zimekatishwa.

Kabla ya tangazo hilo, balozi wa Niger nchini Marekani, Kiari Liman-Tinguiri, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba wanajeshi walijitangazia serikali lazima wafikirie na kutambua kwamba jambo hilo haliwezi kufanikiwa.

Niger ni mzalishaji mkubwa wa madini ya uranium ambayo ni ni muhimu kwa nishati ya nyuklia.

**BBC**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......74/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: GLORIA JOHANES wa KIHONDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA JOHANES SENENGULA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 18 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 31 mwezi 07 mwaka 2023

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BWANA FEDRICK NYALUKE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI MC227 CKS ,RANGI YA LIJANI YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA **IRI/IRI/RB/227282/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......70/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: PHILIPO YOSIA MADETE wa K/NDEGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA JAMES PHILIPO MADETE**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 7 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 07 mwaka 2023

HAKIMU

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahamkama ya mwanzo ya wilaya ya Iringa kituo cha kalenga mkoa wa Iringa**
**Usimamizi wa mirathi namba 6 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HENRY MBINDA WA NZIHI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ELDEFONSI MBINDA.**
**TANGAZO**
**[Kanuni 5[2] ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama ya mwanzo.]**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowowte/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya ivo mnamo tarehe 21 mwezi 08 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji ajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaruhusiwa kuuleta mahakamani kukaguliwa.
.Wosia wa marehemu uyo upo mahakamani na unaweza kukaguiwa
.Marehemu akuacha wosia
.Futa isiyohusika
Imetolewa leo tarehe 31 mwezi 07 2023.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MARY EMMANUEL KAAYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipikiaina ya sinoray yenye usajili namba: MC 129DDV, CHASSIS NAMBA: LD3PCK6J8M2014011 na ENGINE NAMBA: SR162FMJ21094011. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/262263/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA NAMBA 140 YA MWAKA 2022**
**HAMAD SULEIMAN NANJOBE ..............MRUFANI**
**VERSUS**
**MARKY AUGUSTINE MMASY..........1. MJIBU RUFANI**
**MUYA S. BAKARI.......2. MJIBU RUFANI**

**KWA:MUYA S. BAKARI**
**DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mrufani aliyetajwa hapo juu amefungua shauri la maombi ya Rufaa dhidi yako, Maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi hayo zinapatikana katika mahakama hii, hivyo basi, unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 22/08/2023 saa tatu(3:00)asubuhi mbele ya Mhe E.E KAKOLAKI, J. Kujibu madai hayo dhiidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.
ANGALIA
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikathibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
HATI hii imetolewa kwa MKONO wangu na CHAPA ya mahakama leo hii tarehe 28 mwezi 07 2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA MJINI**
**Kituo cha MAKOLE**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 68/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU AMINA ALLY NGALE wa MAKOLE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA SHABANI RAMADHANI TEMBO**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 02 Mwezi 08 Mwaka 2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 52/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU TABU MUSSA BUHETI wa Chamwino Nduka**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA EMMANUEL KAYANDA HOSSEA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 27 Mwezi 07 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA CHETI



**SOME .M. JAPHET** anatangaza kupotelewa na Cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba S.1707-0029 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia Shule ya Sekondari ORKOLILI mwaka 2009.
Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Taarifa ya Polisi: MGZ/RB/767/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya MOSHI**
**Kituo cha KAHE**
**Mkoa KILIMANJARO**
**Usimamizi wa mirathi Na 16/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SAMWEL JOHN SITTA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA AMANI SAMWEL SITTA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 mwezi 08 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 03 mwezi 07 mwaka 2023

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake.

# Maiti kwenye kiroba-**20**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

ILITOKEA kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama waliangua vilio, viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

**************************************

Kitendo cha kuachiwa huru bila kudhuriwa, kulipwa mara mbili ya kazi aliyoifanya kutoka uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, kumpeleka Kawe, halafu kumrudisha hadi Ukonga Banana, na kutoka huko mpaka Kipawa, licha ya kumjumlishia hesabu ya woga, lakini yeye aliamua kulipa mara mbili yake ili kumuonyesha hakuwa mtu mbaya.

Pia alimtahadharisha kuwa asimwambie yeyote tukio lile na siyo kwa sababu ya abiria yule kuogopa, ila kumhofia yeye kama dereva kuuawa au kufanyiwa kitu kibaya na mtu yeyote ambaye angeweza kumuuliza tukio hilo au kumwambia.

Hapo alihofia kuwa jambo lile lingeweza kufika kwa watu ambao wana uhusiano na tukio alilolifanya. Pia, kitendo cha kupiga picha za video na mnato nyumba ya tajiri yake huyo ambaye huwa anamkodisha ilionyesha kuna tukio fulani nyuma ya pazia ambalo yeye hapaswi kuliongea.

"Inawezekana wana bifu lao. Na tajiri yangu yule inaonekana akijua kama kuna mtu nimemleta hapa anaweza kunidhuru." Akawaza hilo na kuamua kufunga bakuli lake.

Siku chache baadaye dereva yule alikodishwa na mtu mmoja ambaye akamkumbuka. Na kweli abiria akamkumbusha kuwa kuna siku walimkodisha kutoka Banana hadi Magomeni.

Dereva akakumbuka kuwa ndiyo ile siku ambayo walikuwa na mzigo. Hata hivyo sauti ya Eddy ikamjia kuwa asimwambie mtu yoyote kuhusu habari ile ya yeye kumpeleka kwenye nyumba ya rafiki yao. Hakusema chochote. Na wala abiria yule hakumuuliza chochote bali walipiga stori za hapa na pale.

Dereva alikuwa na hofu kwani alijua huenda abiria yule amekodisha kwa ajili ya kumuuliza swali linalofanana na hilo.

Alipofika Magomeni, maeneo yale yale ambayo walifikisha mzigo ule, alishuka na kumkaribisha kwenye ukumbi huo akimwambia kila wiki huwa anapatikana humo.

Wiki ya pili dereva yule alikwenda Lango la Jiji na kumuona jamaa yule. Hapo ndipo alipopiga kwenye namba ambayo alipewa na Eddy apige kama kutakuwa na mtu anamsumbua. Ilikuwa namba ya Mary.

Hakuficha kitu kwa sababu namba alipewa na abiria yule ambaye pamoja na kwamba alimuwekea bastola shingoni lakini alimuona hana baya.

Mary aliposikia hivyo alimpigia Eddy, akamuunganisha na dereva taxi yule. Eddy alimtuma dereva akamuangalie tena kwenye baa ile ya Lango la Jiji Magomeni kama huwa anakwenda mara kwa mara.

Akajidhihirisha kuwa kila jioni hufika hapo, huwa haonekani mara moja moja sana.

Eddy akampigia simu Inspekta Frank kwenda kumkamata mtuhumiwa huyo.

Inpekta Frank naye akatuma vijana wake Sajenti Moses na Koplo Ben wakaitekeleza kazi hiyo.

******************************

"Unaitwa nani?"

"Mboneka Fisimaji."

"Okay, unajua mimi ni mstaarabu sana. Siyo kama hao uliokutana nao huko, kwa hiyo nataka unieleze maswali nitakayokuuliza. Sitaki unijibu kwa kunifurahisha, au kujiokoa, nataka ujibu kile tu ambacho unaona ni ukweli unaoufahamu, kama hufahamu sema tu hilo sifahamu. Ila angalizo ni kwamba kama ukinidanganya mimi najua. Na nikidanganywa na kuwa ni hatari mno kuliko hao waliokuchukua."

"Sawa kiongozi." Akajibu kwa sauti ndogo ya woga.

Tayari alikuwa ameshanyooshwa kidogo ili kumlainisha kusema ukweli. Akausema. Hapa Eddy alikuwa anataka aseme akiwa huru mbele ya mitambo ya kamera iliyokuwa ikichukua picha zake, pamoja na picha zingine za mnato.

Mahojiano hayo yalifanyika kwenye ofisi ya Eddy Kamal, mpelelezi maarufu nchini, aliyepewa jukumu la kumsaka muuaji wa mwanamke Tessy.

Aliuawa kikatili kwa kuchinjwa, na kukatwakatwa kama nyama buchani, vipande vyake vikigunduliaka siku tatu baadaye maeneo ya Kinondoni Msisiri vikiwa vimerundikwa kwenye kiroba.

"Unaweza kuniambia siku ambayo dereva taxi alikuja kuwachukua usiku mlikuwa wangapi?"

"Watatu."

"Mlikuwa na nini?"

"Mzigo."

"Mlikuwa mnaupeleka wapi?"

"Magomeni."

"Kwa nani?"

"Hata sijui, tulipofika waliteremka wenzangu wawili, mimi nikarudishwa nyumbani."

"Ulikuwa ni mzigo wa nini?"

Hakujibu haraka.

**Mimi niliwekwa kwenye kochi, wao wakaelekea uani ambako kulikuwa na vyumba vingine huko. Wakakaa kwa muda mrefu sana. Sikuwa nasikia chochote mpaka nikawa nahisi wameondoka. Nikadhani wametokea kwenye mlango wa nyuma.**




"Nimekwambia, usiongope wala kujibu kwa kuogopa, jibu kwa sababu ukijibu vema na ukatusaidia mimi nitawaambia polisi wakuachie."

"Kiongozi mimi niliachwa nje, wao wawili ndiyo walikuwa ndani."

"Kwa hiyo hujui kwenye ndani ya mzigo mlikuwa na nini?"

"Kitu kama maiti hivi."

"Kwa nini unadhani ilikuwa kitu kama maiti halafu huna uhakika?"

"Kuna kitu nilikiona."

"Kitu gani?"

"Nilichungulia dirishani nikaona kitu cha ajabu, lakini nikajifanya sijaona kitu."

Ili ampate vizuri, Eddy alimhamisha eneo hilo kwa sababu alijua anaweza kuzunguka sana asipate kile anachohitaji kwa asilimia mia moja. Na hiyo huwa ni moja kati ya mbinu za wapelelezi wanapowahoji watuhumiwa.

"Wewe ulifikaje pale? Ulipelekwa na nani? Na alikwambia mnakwenda kufanya nini?"

"Nilichukuliwa na anko wangu akaniambia twende sehemu yeye ana dili na rafiki yake. Hakuaniambia anakwenda kufanya nini. Nilipofika kwenye nyumba moja hivi Ukonga Banana tukaingia. Mwenyeji wetu mimi jina simjui, anko wangu alikuwa anamwita Taita, lakini hilo jina walikuwa wanaitana wote kwa sababu hata yeye alikuwa anamwita hivyo anko wangu."

"Baada ya hapo?"

"Mimi niliwekwa kwenye kochi, wao wakaelekea uani ambako kulikuwa na vyumba vingine huko. Wakakaa kwa muda mrefu sana. Sikuwa nasikia chochote mpaka nikawa nahisi wameondoka. Nikadhani wametokea kwenye mlango wa nyuma.

Baada ya kuona kimya sana kama nipo peke yangu, halafu nikawa nashangaa nyumba kubwa na nzuri kama ile kuwa haina mtu, nikanyanyuka na kwenda uani ambako niliona wameelekea."

"Uliwakuta?"

"Nilipofika uani mbele ukumbi mdogo hivi, nikaingia, pembeni kulikuwa na vyumba. Ghafla nilifika kwenye dirisha la chumba kimoja nikaona kitu cha ajabu."

"Kitu gani?"

"Nikamuona mwanamke alikuwa amefungwa mikono na miguu, amefungwa na kitambaa mdomoni, halafu yule mwenyeji wetu akawa na kisu kikubwa, akamfungua miguu na mikono, akaanza kumkata mkono mmoja mmoja mwanamke yule akiwa hai. Mwanamke alionekana kuwa na maumivu makali lakini mwili wake uliokuwa umefungwa kwenye nguzo. Hakuweza kufanya chochote akiwa na wanaume wake wawili."

ITAENDELEA JUMAMOSI

# SINGIDA: SIMBA TUKUTANE TANGA



**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate, Hans Van Pluijm amesema ameridhishwa na kiwango cha wachezaji wake na sasa wapo tayari kuikabili Simba kwenye mchezo wao wa Ngao ya Jamii utakaofanyika Agosti 10 kwenye uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Pluijm amesema kiwango walichokionyesha wachezaji wake kwenye mchezo wao wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya AS Vita uliochezwa Jumatano iliyopita kimemfurahisha na kumemuaminisha kuwa sasa wapo tayari kwa ligi kuu na michezo yote iliyopo mbele yao.

**Mholanzi huyo amesema wachezaji wake walicheza mechi hiyo kwa bidii na kujituma, hivyo ana uhakika kama wataendelea kucheza hivyo kwenye mechi zinazofuata hana shaka na ushindi kwani anaviamini viwango vya wachezaji wake.**

"Wachezaji wangu wamenionyeshea namna walivyo tayari kwa michezo ya ushindani, tuna mchezo dhidi ya Simba hivi karibuni, naamini tupo tayari kukabiliana nao kutokana na ubora wa wachezaji wangu, waliongalia mchezo wetu na As Vita wanaweza kuona namna kikosi kilivyoimarika," alisema Pluijm.

Alipoulizwa juu ya michuano ya kimataifa huku timu yake ikiwa haina uzoefu sana wa michuano hiyo, alisema kikubwa ni maandalizi na kucheza kwa kujiamini tu.

"Kwenye michuano ya kimataifa, timu yangu haina uzoefu sana, lakini muhimu ni kucheza kwa kujiamini, ukijiamini unaweza kumfunga mpinzani wako," alisema Kocha huyo wa zamani wa Yanga.

Singida Fountain Gate inatarajiwa kusafiri kesho kuelekea Tanga tayari kwa mchezo wao wa Jumatano dhidi ya Simba wa kuwania Ngao ya jamii.

Singida ikifanikiwa kuifunga Simba itakutana na mshindi wa mchezo kati ya YAnga na Azam kwenye fainali kuwania ngao hiyo msimu huu.

# *Minziro aitabiria makubwa Prisons*

**Na Abdallah Mataka**

KOCHA mpya wa Tanzania Prisons, Fred Minziro amesema kwa mechi za kirafiki alizocheza ameona mabadiliko makubwa kwa wachezaji wake na anaamini watatoa ushindani mkubwa kwenye ligi.

Minziro alisema ushiriki wa timu hiyo kwenye mashindano ya 'Samia Mbeya Nane Nane 2023' yamempa mwanga wa kuona uimara wa timu yake.

Alisema kwa sasa anarekebisha vitu vichache vya kiufundi na baada ya hapo watakuwa tayari kwa msimu mpya wa ligi kuu unaotarajiwa kuanza Agosti 15.

"Tumecheza zaidi ya mechi tatu za kirafiki zikiwemo zile za mashindano ya nane nane, kikosi naona kimeimarika lakini yapo mambo machache ambayo kwa siku hizi zilizobakia tutayafanyia kazi, naamini timu yangu itatoa ushindani mkubwa kwenye ligi," alisema Minziro.

Alisema atapambana kuhakikisha timu yake inafanya vizuri zaidi msimu huu kwenye ligi tofauti na msimu uliopita ambao hawakufanya vizuri.

Katika mashindano ya Sambia Mbeya nanene, Minziro licha ya kusaidia timu yake kuibuka mabingwa, pia alichaguliwa kuwa kocha bora wa michuano hiyo maalum.

" Hikuwa rahisi ilikuwa kazi ngumu lakini namshukuru mwenyezi mungu ameona ni jinsi gani Prison tumejiandaa yote kwa yote kwa kuanza vizuri kazi kwenye timu hii," alisema Minziro.

Mashindano hayo yalishirikisha timu nne za Prisons, Mbeya Kwanza, Mbeya City na wageni waalikwa Baka City kutoka Malawi ambao walishika nafasi ya pili nyuma ya mabingwa Prisons.



Katibu Mkuu wa Klabu ya Geita Gold, Simon Shija (Kulia) na Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania, Erick Gerald, wakibadilishana hati ya mkataba wa udhamini waliousaini juzi, hafla ya utiaji saini ilifanyika mjini Geita. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Tabora Utd yashusha 'vyuma'

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United imekamilisha rasmi usajili wake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kupata saini za wachezaji kutoka nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ikiwemo TP Mazembe, Botswana, Burundi na Nigeria.

Akizungumza jiji Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo Henry Mkama amesema wamefanya usajili wa nguvu ambao wanaamini utaleta chachu kubwa kwenye soka la Tanzania, huku wakiwa wana jumla ya wachezaji 26, wazawa 14 na wageni 12.

Kocha huyo aliwataja baadhi ya wachezaji wapya waliowasajili kwa ajili ya msimu ujao kuwa ni John Noble kutoka Nigeria, Mutuale Nyongani kutoka Maniema ya DR Congo, Lumiere Banza Kalumba (TP Mazembe), Andy Bikoko Lobuka Sanga (Balende FC- DR Congo), wengine nin kiungo mshambuliaji Toauya Jean Didie kutoka Rajaa FC ya Burundi na Kelvin Kingu Pemba kutoka Mbabane Swallows ya Eswatini.

"Hali za wachezaji wetu wote ziko vizuri, wanaendelea na mazoezi chini ya kocha wetu Goran Kuponovic," alisema Mkama.

Aidha, Ofisa habari wa klabu hiyo Pendo Lema, alisema usajili walioufanya ni usajili mkubwa na wenye tija na utakwenda kuleta ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Tabora United itacheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu ujao utakaanza Agosti 15 baada ya kupanda daraja msimu uliopita wakati ikijulikana kama Kitayosce FC.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## MAGUIRE KUTUA EVERTON

EVERTON imewapiku Tottenham Hotspur na West Ham katika mbio za kumsajili beki wa Manchester United na England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30. ***(Football Insider)***

## LOPETEGUI ANATAFAKARI

KOCHA wa Wolves, Julen Lopetegui anatafakari kuhusu nafasi yake kama kocha wa klabu ya Midlands. ***(Mirror)***

## MICHAEL OLISE AGOMBEWA

Chelsea na Manchester City zinaongeza juhudi zao za kumsajili winga wa Crystal Palace, Mfaransa Michael Olise mwenye umri wa miaka 21, huku kukiwa na mkanganyiko kuhusu kipengele cha kutolewa katika mkataba wake. ***(Mirror)***

## RAMOS AKARIBIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inakaribia kumpata mshambuliaji wa Benfica na Ureno, Goncalo Ramos, 22, kwenye klabu hiyo. ***(L'Equipe)***

## LENGLET HAITAKI SAUDIA

CLEMENT Lenglet, 28, anapinga mpango wa Barcelona wa kumuuza kwa klabu ya Saudia ya Al-Nassr - huku beki huyo wa Ufaransa akidhamiria kurejea Tottenham, ambako alicheza kwa mkopo msimu uliopita. ***(Sport)***

## CHELSEA NA LUKAKU

MATUMAINI ya Chelsea kubadilishana mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 30 na mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic, 23, katika mkataba wa mchezaji pamoja na fedha, yamekatishwa tamaa na matakwa ya wababe hao wa Italia ya kutaka ada ya pauni milioni 35. ***(Star)***

## GORETZKA AWINDWA MAN

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kiungo wa Bayern Munich na Ujerumani, Leon Goretzka, 28, ambaye tetesi zinadai hayuko katika mipango ya kocha Thomas Tuchel. ***(Mail)***

## A'VILLA KUMCHUKUA ADAMS

ASTON Villa iko tayari kutumia kipengele cha kuachiliwa kwa kiungo wa Leeds United, Tyler Adams, 24 cha pauni milioni 25 na wanasubiri jibu kutoka kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani kuhusu mustakabali wake, huku Chelsea pia wakifikiria kumnunua. ***(Mail)***

## SPURS KUTOA NYOTA

KLABU ya Tottenham Hotsput inajadili kuhusu usajili wa mshambuliaji wa Argentina mwenye thamani ya pauni milioni 12, Alejo Veliz, 19, kutoka Rosario Central - na wanatazamia kuwatoa kipa wa Ufaransa, Hugo Lloris mwenye miaka 36 na kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 27, Mfaransa Tanguy Ndombele mwenye miaka 26 na winga wa Hispania, Bryan Gil, 22. ***(Evening Standard)***

## DEMBELE SAFI PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 26 jana Ijumaa alifanyiwa vipimo vya afya kabla ya kukamilisha uhamisho kutoka Barcelona kwenda Paris St-Germain. ***(RMC Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MADDISON: NATAKA KANE ABAKI HOTSPUR

**LONDON,** England

JAMES Maddison angependa Harry Kane abaki Tottenham Hotspur lakini amesisitiza kuwa uvumi unaoendelea kuhusu fowadi huyo haujawasumbua wachezaji wenzake wapya.

**Maddison alikua mmoja wa wachezaji wa kwanza kusajiliwa chini ya kocha mpya, Ange Postecoglou pale Spurs ilipokamilisha uhamisho wa pauni milioni 40 kutoka Leicester mwezi uliopita.**

Wiki tano zimepita na bado mustakabali wa Kane haujajulikana, huku Bayern Munich wakiwa na nia ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England na wanatarajiwa kuwasilisha ombi jipya kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

●●● Asema hata hivyo uvumi wa mshambuliaji huyo kutakiwa na klabu nyingine...

Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy aliripotiwa kukutana na maofisa wa Bayern mjini London Jumatatu na ziara ya hivi majuzi ya klabu hiyo katika bara la Asia-Pacific ilitokea huku kukiwa na mazungumzo ya mara kwa mara kuhusu mustakabali wa Kane, na mwandishi wa habari wa Bild alithibitisha jezi ya Bayern na Kane yenye namba 9 mgongoni kwa Postecoglou wakati wa mkutano na waandishi wa habari.

Lakini Maddison, akizungumza kwenye hafla ya kuanza kwa msimu wa TNT Sports huko London, alisema: "Haijakuwa kikwazo, Harry ni mtaalamu wa hali ya juu.

"Sitaelezea kwa undani kwa sababu sijui chochote na tuwe na heshima kuhusu hali ya Harry.

"Kila mtu anajua Harry Kane ni mtu wa namna gani, yeye ni mtaalamu wa hali ya juu na klabu yoyote aliyopo, wakati wowote anapoingia kwenye mazoezi hutoa asilimia 100 ya nguvu zake.

"Tulikuwa marafiki kabla sijajiunga na Tottenham tukiwa kikosi cha England.

"Ningependa Harry Kane abaki. Yeye ndiye namba tisa bora zaidi duniani kwa maoni yangu, lakini itakuwaje akiondoka.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,139,8

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
LENS
1 | 1.58
X | 3.77
2 | 4.99

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AL AHLI YAZIPIKU JUVE NA SPURS KUMSAJILI




**RIYADH,** Saudi Aarabia

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Franck Kessie anakaribia kuhamia klabu ya Al Ahli ya Saudi Arabia, vyanzo vimeithibitishia 90min.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast alijiunga tu na Barca kutoka AC Milan kwa uhamisho wa bila malipo msimu uliopita wa joto, na licha ya kufunga bao la ushindi la kukumbukwa dakika ya mwisho dhidi ya Real Madrid wakiwa njiani kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, hakupewa nafasi nyingi zaidi pale Camp Nou.

90min iliripoti Jumatano kwamba Tottenham ilifanya mazungumzo na Barcelona juu ya kumsajili Kessie pamoja na mchezaji mwenzake, Clement Lenglet, ambaye alitumia msimu uliopita kwa mkopo kaskazini mwa London.

Lakini Spurs watamkosa Kessie kwani amekubali kujiunga na Al Ahli.

Barcelona awali walidhani kwamba upendeleo wa Kessie ni kubaki Ulaya, lakini sasa watakaa chini na kuwapiku Al Ahli ili kupata euro milioni 15, ambao pia wamewasajili Edouard Mendy, Roberto Firmino, Riyad Mahrez na Allan Saint-Maximin katika dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto.

Kikubwa zaidi, Barcelona hawatalazimika kulipa sehemu ya mishahara ya Kessie ili kumwondosha kwenye vitabu vyao, hivyo kuwawezesha kubadilika zaidi chini ya vikwazo vikali vya kifedha vya LLiga.




# Brighton yaikazia Chelsea

**LONDON,** England

KLABU ya Brighton & Hove Albion imeweka wazi kuwa Moses Caicedo hatauzwa isipokuwa kama dau lao la pauni 100 itafikiwa, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ecuador anaendelea kuwindwa na Chelsea, ambayo tayari imeshuhudia ofa mbili - ya kwanza yenye thamani ya pauni milioni 70 na ya pili yenye thamani ya pauni milioni 80 - ikikataliwa na Seagulls hao.

90min inaelewa kuwa Caicedo amethibitisha nia yake ya kutaka kuondoka Brighton mara kadhaa msimu huu wa joto.

Brighton inamthaminisha Caicedo kwa kiasi sawa na Declan Rice, ambaye alisajiliwa hivi karibuni na Arsenal kutoka West Ham United kwa ada ya uhamisho ya rekodi ya England ya pauni milioni 105.

Chelsea bado haijakata tamaa katika harakati zake za kumnasa Caicedo na itaendelea kusonga mbele.

Tayari imekubali dili la kumsajili Robert Sanchez kutoka Brighton dirisha hili la joto.

Alipoulizwa masw[...] kuhusu Caicedo kabla [...] mechi yao ya kirafiki [...] kujiandaa na msimu mp[...] dhidi ya Chelsea nch[...] Marekani mwezi uliop[...] kocha mkuu wa Bright[...] Roberto De Zerbi alisisit[...] kuwa kiungo huyo [...] taendi popote hivi karibu[...] na akadhihaki kushind[...] kwa The Blues hao kufu[...] Ulaya.

"Ni hali ya wazi kwa sa[...] Caicedo anabakia nasi h[...] mmiliki wangu abadilis[...] mawazo yake," alisema [...] Zerbi.

HABARI MICHEZO

359,317/-

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/23 | 13:00 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama Marinos | 2.23 | 3.35 | 2.70 |
| 02. 06/08/23 | 13:00 | Kyoto Sanga FC vs Kashiwa Reysol | 2.22 | 3.05 | 2.90 |
| 03. 06/08/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Avispa Fukuoka | 2.40 | 3.00 | 2.70 |
| 04. 06/08/23 | 13:00 | Thespakusatsu vs Tochigi SC | 2.75 | 2.90 | 2.45 |
| 05. 06/08/23 | 13:00 | Omiya Ardija vs Blaublitz Akita | 2.65 | 2.95 | 2.46 |
| 06. 06/08/23 | 13:00 | Tokushima Vortis vs JEF United Ichihara Chiba | 2.85 | 3.05 | 2.27 |
| 07. 06/08/23 | 14:30 | Karlsruher SC vs Hamburger SV | 2.90 | 3.70 | 2.16 |
| 08. 06/08/23 | 14:30 | 1 FC Nuremberg vs Hannover 96 | 2.16 | 3.55 | 3.00 |
| 09. 06/08/23 | 14:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 10. 06/08/23 | 16:00 | Kalmar FF vs AIK | 2.55 | 3.00 | 2.55 |
| 11. 06/08/23 | 16:00 | FK Teplice vs FK Jablonec | 2.60 | 3.20 | 2.37 |
| 12. 06/08/23 | 17:30 | Grasshopper Club Zurich vs FC Basel 1893 | 2.75 | 3.45 | 2.16 |
| 13. 06/08/23 | 18:00 | FK Haugesund vs Rosenborg BK | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 14. 06/08/23 | 18:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.27 | 3.25 | 2.70 |
| 15. 06/08/23 | 18:00 | Blau-Weiss Linz vs TSV Hartberg | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 16. 06/08/23 | 19:00 | Sunderland AFC vs Ipswich Town | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 17. 06/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.40 | 2.33 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 05/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3794 | Tanjong Pagar United FC vs Young Lions | 1.67 | 4.54 | 3.43 |
| 14:00 | 4526 | SV Elversberg vs Hansa | 2.20 | 3.41 | 3.01 |
| 14:00 | 5915 | FC Elva vs FC Tallinn | 2.61 | 3.82 | 2.35 |
| 14:30 | 1418 | Celtic vs Ross County | 1.10 | 8.53 | 16.86 |
| 14:45 | 5520 | Manchester Utd vs Lens | 1.58 | 3.77 | 4.99 |
| 15:00 | 1675 | Kryliya Sovetov vs Rostov | 2.32 | 3.23 | 2.87 |
| 15:00 | 2751 | Persepam MU vs Psis Semarang | 1.93 | 3.43 | 3.33 |
| 16:00 | 1867 | Landskrona Bois vs Ostersunds | 2.22 | 3.40 | 3.08 |
| 16:00 | 1897 | Gefle IF vs IK Brage | 2.99 | 3.46 | 2.24 |
| 16:00 | 2932 | SuperSport Utd vs Richards Bay FC | 1.68 | 3.25 | 5.36 |
| 16:00 | 3361 | St Etienne vs Grenoble Foot | 1.60 | 3.80 | 4.94 |
| 17:00 | 1156 | St Johnstone vs Hearts | 2.99 | 3.43 | 2.18 |
| 17:00 | 1228 | Livingston vs Aberdeen | 2.80 | 3.20 | 2.41 |
| 17:00 | 1369 | Blackburn vs West Bromwich | 2.68 | 3.12 | 2.53 |
| 17:00 | 1542 | Dundee FC vs Motherwell | 2.50 | 3.25 | 2.65 |
| 17:00 | 1769 | Plymouth vs Huddersfield | 2.15 | 3.27 | 3.12 |
| 17:00 | 2510 | Partick Thisle vs Raith Rovers | 2.10 | 3.47 | 3.01 |
| 17:00 | 2608 | Copenhagen vs Randers | 1.29 | 5.22 | 9.44 |
| 17:00 | 2634 | Bristol City vs Preston | 2.03 | 3.27 | 3.42 |
| 17:00 | 2780 | Racing Genk vs Eupen | 1.27 | 5.57 | 8.35 |
| 17:00 | 3259 | Inverness vs Queens Park | 2.25 | 3.47 | 2.76 |
| 17:00 | 3512 | Morton vs Ayr United | 2.10 | 3.47 | 3.01 |
| 17:00 | 3610 | Middlesbrough vs Millwall | 1.91 | 3.33 | 3.77 |
| 17:00 | 3812 | Stoke City vs Rotherham | 1.63 | 3.63 | 4.97 |
| 17:00 | 4703 | Watford vs QPR | 1.90 | 3.41 | 3.71 |
| 17:00 | 4983 | SC Bruhl vs BSC Young Boys | 1.77 | 3.80 | 3.40 |
| 17:00 | 5045 | Norwich City vs Hull City | 1.69 | 3.60 | 4.54 |
| 17:00 | 5178 | Swansea vs Birmingham | 1.82 | 3.47 | 3.96 |
| 17:30 | 1113 | Newcastle vs Fiorentina | 1.58 | 3.97 | 4.68 |
| 17:30 | 5714 | Rubin Kazan vs Spartak Moscow | 3.18 | 3.48 | 2.05 |
| 18:00 | 4012 | Rapid Vienna vs SCR Altach | 1.48 | 4.12 | 5.23 |
| 18:30 | 3294 | Bloemfontein Celtic vs Amazulu | 2.34 | 3.02 | 3.02 |
| 19:00 | 2487 | Catanzaro vs Foggia | 1.20 | 6.47 | 11.48 |
| 19:00 | 2752 | Stromsgodset vs Valerenga | 2.23 | 3.45 | 2.88 |
| 19:15 | 1218 | Cercle Brugge vs Charleroi | 1.84 | 3.69 | 3.69 |
| 19:15 | 2212 | Kilmarnock vs Rangers | 6.16 | 4.67 | 1.41 |
| 19:45 | 4095 | Slaven Belupo vs Rudes Zagreb | 1.86 | 3.43 | 3.58 |
| 20:00 | 2316 | Laval vs Angers | 2.56 | 3.10 | 2.66 |
| 20:00 | 3280 | Valenciennes vs AJ Auxerre | 3.36 | 3.26 | 2.06 |
| 20:00 | 3740 | CSKA Moscow vs Lokomotiv Moscow | 2.03 | 3.54 | 3.18 |
| 20:00 | 4987 | Paris FC vs Caen | 2.38 | 3.17 | 2.82 |
| 20:30 | 4381 | Sturm Graz vs LASK Linz | 1.65 | 3.74 | 4.25 |
| 21:00 | 2708 | FK Zeleznicar Pancevo vs Mladost Lucani | 2.30 | 3.12 | 2.82 |
| 21:00 | 3006 | Stellenbosch vs Orlando Pirates | 3.18 | 3.03 | 2.25 |
| 21:05 | 4521 | Red Star Belgrade vs FK Napredak | 1.07 | 8.85 | 17.09 |
| 21:30 | 1824 | FC Zurich vs FC Lugano | 2.21 | 3.41 | 2.95 |
| 21:30 | 2360 | Universitatea Cluj vs Dinamo Bucuresti | 1.92 | 3.29 | 3.75 |
| 21:30 | 4562 | Schalke 04 vs Kaiserslautern | 1.64 | 3.86 | 4.71 |
| 22:00 | 1685 | Dinamo Zagreb vs HNK Gorica | 1.24 | 5.05 | 9.30 |
| 22:00 | 4242 | Valencia vs Aston Villa | 3.10 | 3.46 | 2.05 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# AJIBU ATAMBULISHWA RASMI COASTAL UNION

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya tetesi za muda mrefu, hatimaye klabu ya Coastal Union imemtambulisha rasmi kiungo mshambuliaji Ibrahim Ajibu kutoka Singida Fountain Gate.

**Taarifa ya klabu hiyo iliyotolewa jana inasema Ajibu amesajiliwa kwa mkataba wa miaka mwili ambapo wana matumaini atafanya makubwa chini ya kocha aliyewahi kuwa naye huko nyuma, Mkongomani, Mwinyi Zahera.**

"Tunayo furaha kumtangaza 'Mzee wa Makorokoro' Ibrahim Ajibu kuwa ni mchezaji wetu," iliandika sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Uongozi wa klabu hiyo umesema wana imani kuwa Ajibu atafanya vyema kwenye kikosi chao kwa sababu yupo chini ya kocha aliyemfanya kucheza kwa kiwango cha juu wakati wote wakiwa waajiriwa wa klabu ya Yanga.

Ajibu ni zao la kikosi cha pili cha Simba ambayo ilimpeleka kwa mkopo katika klabu ya Mwadui FC 2016, kabla ya kurejeshwa na kupandishwa kikosi cha kwanza 2017.

Hata hivyo, alijiunga na Yanga 2019 ambako alicheza kwa mafanikio makubwa chini ya Zahera, kabla ya kurejea kwenye klabu yake ya zamani, Simba 2021.

Alidumu Simba kwa nusu msimu kabla ya kujiunga na Azam FC ambako nako alikaa hadi nusu ya msimu uliopita alipoibukia Singida Fountaine Gate.

Mbali na Ajibu, Coastal ambayo msimu uliopita ilipigania uhai wa kubaki Ligi Kuu hadi dakika za mwisho imemsajili winga Lucas Kikoti kutoka Namungo FC na Ally Kombo aliyekuwa akiichezea Ruvu Shooting.



Mshambuliaji wa timu ya Don Bosco Veteran ya Oysterbay, Khalid Kajuna (katikati), akiwatoka wachezaji wa Tnt Island, katika mechi ya kirafiki uliyochezwa juzi Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jui. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba kuwashangaza mashabiki Simba Day

ENDELEA UKURASA 23

Taarifa zinasema Simba ipo kwenye hatua za mwisho kumsajili golikipa mpya kuchukua nafasi ya Mbrazil Jefferson Luis ambaye waliachana naye kutokana na kipa huyo kuumia akiwa kwenye kambi ya timu hiyo nchini Uturuki.

"Suala la golikipa limeshakamilika, mashabiki watamuona siku ya tamasha letu, ni golikipa mwenye viwango vikubwa ambaye anakuja kuongeza kitu nadani ya klabu yetu," alisema Ahmed bila kutaja jina la kipa huyo.

Aidha, alisema kwa kuwa kuna mambo makubwa wanatarajia kuyafanya siku ya tamasha na kuwataka mashabiki kufika mapema uwanjani kushuhudia.

"Sisi ni wa kwanza kwenye mambo haya na siku zote tutaendelea kuwa juu, waje wajifunze namna ya kuandaa matamasha, kila atakayekuja kwenye siku yetu atafurahia kila kitu," alisema Ahmed.

Katika kilele cha tamasha hilo pia Simba inatarajia kucheza mchezo wa kimataifa wa kirafiki na klabu ya Power Dynamos ya Zambia.

Katika hatua nyingine, uongozi wa klabu hiyo umesema wameweka taarifa zao zote kwenye jumba la makambusho la taifa kwa ajili historia kwa vizazi vijavyo.

Ahmed alisema wameshirikiana na wasomi na wataalamu wa makumbusho hayo ya taifa ili kuweka historia ya timu hiyo.

"Kuleta jambo letu kwa wataalamu na wasomi ni kwa sababu ya kutunza kumbukumbu za Simba, hatuwezi kutengeneza filamu, mambo yetu yote ikiwemo kibegi na kiatu cha bao bora la msimu 2021/22 kwenye kombe la Shirikisho Afrika alichotwaa mshambuliaji wetu, Pape Ousmane Sakho kitakuwa sehemu ya nyumba hii ya Makumbusho," alisema Ahmed.

Michezo
Jumamosi Agosti 5, 2023
Nipashe



Brighton yaikazia Chelsea kwa Caicedo UKURASA 22




Wachezaji wa zamani wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto (Kulia) na Yanick Bangala wakiwania mpira kwenye mazoezi ya timu yao mpya ya Azam FC jana kujiandaa na mchezo wa Ngao ya jamii dhidi ya timu yao hiyo ya zamani utakaochezwa Jumanne uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. **PICHA: BINZUERY**

SUALA LA GOLIKIPA

# Simba kuwashangaza mashabiki Simba Day

Na Saada Akida

● ● ● Kumtangaza golikipa mpya siku hiyo, watoa sababu kumualika Samia…

UONGOZI wa Klabu ya Simba umesema utawafanyia 'Suprise' mashabiki wao kwa kumtangaza golikipa mpya kwenye tamasha lao la 'Simba Day' litakalofanyika kesho Uwanja wa Benjamin Mkapa huku wakisema ukubwa wa timu yao ndio sababu ya kumualika Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni rasmi.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema Simba Day ya mwaka huu ni kubwa na maalum na sikukuu, hali iliyopelekea kumuomba Rais Dk. Samia kuwa mgeni rasmi.

**Alisema uongozi wa Simba unamshukuru Rais Samia kukubali mwaliko wao na kuwa miongoni mwa watanzania 60,000, watakao hudhuria Simba Day mwaka huu ambayo itakuwa ya aina yake.**

"Maandalizi ya Tamasha hili la historia yanaendelea vizuri, kila kitu kipo kwenye mstari huku taratibu zikiwa vizuri na kusubiriwa siku yenyewe kufika ili mashabiki kupata burudani siku hiyo kuanzia kwa wasanii na mechi mbalimbali za kirafiki ambazo zitachezwa na timu zote za Simba kuanzia ile ya vijana, ya wanawake na timu kubwa," alisema Ahmed.

Aidha, alisema watatumia tamasha hilo pia kutambulisha wachezaji wake wapya huku pia wakiwafanyia 'Suprise' mashabiki wao kwa kumtambulisha golikipa wao mpya.

ENDELEA UKURASA 23

# Yanga: Tunaifuata Ngao yetu Tanga

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha Yanga kinatarajiwa kwenda Tanga Jumatatu kwa ajili ya michuano ya Ngao ya Jamii huku benchi la ufundi likiweka wazi kuwa wanaifuata Ngao yao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe alisema kikosi chao kitaondoka Jumatatu kwa ndege kwenda Tanga na kitafika siku hiyo na kupata mapumziko, kabla ya kufanya mazoezi Jumatano.

"Kikosi kitaelekea Tanga Jumatatu, tutakuwa na siku moja ya mazoezi siku ya Jumanne na, Jumatano ndiyo tutacheza pambano letu dhidi ya Azam FC," alisema Kamwe.

Kamwe alisema benchi la ufundi chini ya kocha Miguel Gamondi amewahakikishia wanaenda kufuata taji hilo la Ngao ya jamiina kurudi nayo Dar es salaam.

"Kila kitu kipo sawa, benchi la ufundi limetuambia kikosi kipo tayari sasa kuifuata ngao yetu, tunaenda Tanga kuendeleza furaha yetu pale tulipoishia msimu uliopita," alisema Kamwe.

Aidha, aliwataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo mikoa ya Pwani, Kilimanjaro na Arusha kufurika kwa wingi uwajani ili kuwapa hamasa wachezaji ambao watakuwa wanaanza kazi ya kutetea mataji yao waliyoyapata msimu uliopita.

"Niwaambie wanachama na mashabiki wa Yanga wa mikoa ya jirani na Tanga wajitokeze kwa wingi, Jumatano ni siku yetu ya kwenda kuujaza uwanja wa Mkwakwani, waje wawape sapoti wachezaji wao," alisema Kamwe.

Alisema kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya mikikimikiki ya meimu mpya na michezo hiyo ya Ngao ya jamii ni ufunguzi kuelekea kwenye ligi itakayoanza Agosti 15

Yanga itacheza mechi ya Ngao ya Jamii Jumatano ijayo dhidi ya Azam FC kabla ya siku ya Alhamisi, Simba kushuka uwanjani hapo dhidi ya Singida Fountaine Gate.

Mshindi wa kila mchezo watakutana kwenye fainali kuwania taji hilo kwa msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >